# *Ishara Mbegu Ya Wakati Wa Mwisho*

Asante, Bwana.

2 Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kuwa hapa usiku wa leo, tena, huku—huku Tifton. Kidogo hili ni jambo la kushangaza sana kwangu. Nilikuwa nimemwambia rafiki yetu mwema Ndugu Welch Evans, wakati fulani uliopita nilipokuwa ninachoka kidogo, nikasema, "Ninashuka kupitia Tifton kwenda kuvua samaki." Nami nikasema, "Nitakapokuja, nitakutana nawe huko mahali fulani, nasi tutakuwa na," niliwaza, "mkutano wa maombi ya kibandani." Na hapa yeye . . . Ninajikuta hapa kwenye ukumbi wa shule usiku wa leo.

3 Na kidogo nimepwelewa na sauti kutoka—kutokana na kuongea kupita kiasi. Nilikuwa na mahubiri mafupi jana, yote ni muda wa saa sita tu, muda niliohubiri. Kwa hiyo, sasa, siwatishi, sitachukua muda mrefu hivyo usiku wa leo, nina hakika na hilo.

4 Lakini kwa kuwa kidogo nimepwelewa na sauti na—na nikipitia huku, lakini ni majaliwa kuwa hapa na kuweza kukutana na mchungaji huyu mwema ambaye alitoa utangulizi mzuri sana, wa kifalme, nasi tuna furaha sikuzote kukutana na watu.

5 Na usemi ambao huyu ndugu ametoa sasa hivi ni wa kweli kabisa, tunaweza kusema, "Amina," kwake, kwa sababu ibilisi, katika siku hizi za mwisho, ni kama simba angurumaye, akizunguka-zunguka akimeza chochote anachoweza kupata cha kumeza, kwa maana anajua muda wake ni mfupi. Hana muda mrefu zaidi wa kufanya hivyo, kwa hiyo hana budi kulifanya wakati akiwa na muda wa kulifanya.

6 Ninapenda mandhari ya jumba hili dogo la mikutano. Ninashukuru sana halmashauri ya shule, mkuu wa shule, na wale ambao wamekuwa wema sana kuturuhusu kuutumia, kwa ajili yenu ninyi watu wazuri mlioko hapa katika ushirikiano kwa ajili ya maskini mkutano huu uliopangwa haraka sana. Na yeyote yule aliyeweka huo mkeka mdogo wa makaribisho hapa nje mtaani, niliuona, vema, hilo lilikuwa zuri sana, nafikiri Ndugu Willie *hapa* ndiye, aliyefanya hivyo, nami ninathamini hilo.

7 Ningependa, labda, kama Bwana akipenda, wakati mwingine ambapo tungeweza kupitia hapa kwa ajili ya msimu wa ibada, tukutane na mchungaji huyu mzuri na wengine hapa, na kuandaa mkutano kwa siku nne ama tano usiku, ambapo tungeweza kuutangaza vya kutosha, tuyalete makanisa

yote pamoja, kwa sababu, mwajua, tunahitajiana mmoja kwa mwingine sasa hivi, zaidi ya tulivyowahi kuwa katika historia yote ya ulimwengu ni sasa hivi, waaminio halisi wa kifalme, tunahitajiana mmoja kwa mwingine. Na kwa hiyo mimi... Daima ni baraka popote uendapo na kukutana na watu wa Mungu, ni baraka kila mahali.

8 Ninaona tuna vijana hapa nje. Nilikuwa nikimwangalia mvulana na msichana mdogo wameketi hapa dakika chache zilizopita kwenye kiti cha mbele, jamaa wadogo warembo sana, maskini jamaa wadogo, wameketi hapo juu vizuri tu; ninapenda hilo. Watoto, kuna kitu fulani kuhusu watoto ambacho hakina hatia na ni kitamu, na—napenda hilo.

9 Na sasa, asanteni sana kwa kujitokeza usiku wa leo. Sasa, nilifikiri ya kwamba lingekuwa ni jambo jema, usiku wa leo, kama tungechukua tu wakati wetu, na kupanda Mbegu fulani ambayo... ya Neno la Bwana. Na jana nilihubiri saa hizi sita juu ya somo: *Mbegu Asili Ya Neno*. Nasi tulilileta kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, huku na huku kwenye kanda ya saa sita kwamba, mpango wa Mungu ulikuwa nini, kile Yeye alicho, na jinsi ambavyo Neno lililonenwa la Mungu ndilo Mbegu ya Mungu, nayo Biblia ilisema ya kwamba, katika Luka, ya kwamba Neno la Mungu ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda.

10 Na sasa, tunajua ya kwamba neno lolote lililopandwa halina budi kutiwa maji kabla halijazaa mazao yake. Lakini kama maji yakianguka ardhini, haidhuru ni mbegu ya aina gani iliyo katika ardhi hiyo, itazaa kwa jinsi yake, maana Mungu alisema katika Mwanzo 1:11, "Kila mbegu na izae kwa jinsi yake. Kwamba kila kitu..." Basi maji yanapoanguka, Waebrania, mlango wa 6, tunaona ya kwamba m—mvua huja mara kwa mara juu ya nchi kuinywesha, kuitayarisha, ipate kuzaa matunda, bali magugu na michongoma, na—na vitu vilivyomo ardhini vinachipuza kwa maji yale yale, lakini, "Kwa matunda yao mnatambulikana."

11 Kwa hiyo Wakristo wanatambulikana kwa matunda ya Roho Mtakatifu, hilo ndilo linaloyatawala maisha ya Mkristo, linathibitisha kile alicho. Nalo tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, imani, uvumilivu, fadhili, utu wema, upole..., subira katika Roho Mtakatifu, matunda hayo yanajidhihirisha kupitia kwa Wakristo.

12 Sasa, tuliona jana, ya kwamba mle ndani ya kwamba ile mbegu iliyopandwa, ile mbegu ya ugomvi, huyo alikuwa ni Shetani aliyepanda ugomvi alipomwambia Hawa uongo. Nasi tunaona kutokuamini Neno moja la Mungu, lililonenwa, kulisababisha kila kifo kilichopata kuwako, kila ugonjwa, na shida hizi zote, kutokuamini tu Neno moja. Yeye *hakuliamini* hasa, alijaribu kuchanganya jambo fulani Nalo, wala hakuna kitu kitakachochanganyikana na Neno la Mungu, Halina budi kuwa hivyo, kwa sababu ndilo Mbegu ya asili.

13 Mungu ni wa Milele, na Mungu ni Neno, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili miongoni mwetu.”

14 Sasa, Mungu na Neno Lake ni Mtu yule yule; liwazieni. Ninaamini ya kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu siku moja, si kwa sheria ya Bunge, si kwa sheria ya kanisa, bali kwa Neno Lake, Yeye atauhukumu ulimwengu. Kama ilitubidi kuchukua kanisa, kanisa la kimadhehebu, ni lipi kati ya hayo lililo sahihi? Yanatofautiana sana moja na lingine. Katoliki inatofautiana na Protestanti, Protestanti inatofautiana na othodoksi, oth-. . . Mbona, kila mmoja tunatofautiana, kwa hiyo ni lipi kati yao lingekuwa sahihi? Tungechanganyikiwa niani mwetu sikuzote, mtu asingejua la kufanya. Naye Mungu mwenye haki, Hakimu wa dunia nzima, hakika atatupa kitu cha kuhukumiwa kwacho.

15 Sasa, ninasoma katika Biblia ya kwamba Mbingu na nchi zitapita, bali Neno la Mungu halitapita kamwe. Ninasoma katika Biblia ya kwamba mtu yeyote atakayeondoa lolote Kwake ama kuongeza lolote Kwake, huyo ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima, kwamba Hicho kinasimama tu jinsi kilivyo.

16 Wengi hujaribu kusema, “Kimebadilishwa, kimefanywa *hivi* ama *vile*.” Siamini hilo, Ninaamini inabidi kuwe na namna fulani ya Kigezo ambacho Mungu atahukumu ka—kanisa kwacho, ama, ulimwengu. Inabidi kuwe na Kigezo fulani, hakiwezi kuwa katika madhehebu ya kanisa, kwa sababu yanatofautiana. Ni nani angejua la kufanya?

17 Lakini kuna Kigezo, na hicho ni Neno Lake. Ninaamini ya kwamba Mungu hulilinda Neno Lake, ninaamini ya kwamba Neno hilo limeandikwa jinsi Mungu anavyolitaka, Biblia; Ni Neno la Mungu kwa wa—watu. Hapo ndipo, ndiyo sababu ya mimi kuliamini Neno hilo. Nami ninaamini Neno ni Mbegu, na kama Mbegu hiyo ikipandwa kwenye udongo mzuri na kumwagiliwa maji na Roho Mtakatifu, itazaa kwa jinsi Yake. Ahadi yoyote ambayo Mungu alitoa, Mungu ataitimiza.

18 Tunapomwona Mungu akimponya mtu. . . Hapa siku chache zilizopita kanisani mwetu, nilikuwa nimetangaza ya kwamba ningehubiri kule Jumapili, Jumapili iliyopita, ni juma moja sasa, juma moja kutoka Jumapili iliyopita. Walimleta msichana mdogo mle ndani kwa machela, nao walikuwa wamenipigia simu usiku barabarani na kusema, “Huyo msichana hawezi kuishi,” hiyo kansa ilikuwa mbaya sana, mwenye umri wa kama miaka kumi na saba, “hata hawezi kufika kule, atakufa kabla hajafika kule.” Kilikuwa ni kisa cha kuhuzunisha, maskini mtoto mdogo wa kupendeza mwenye umri wa miaka kumi na saba.

19 Kuthibitishia kanisa langu jambo fulani, kamwe sikumgusa huyo mtoto hata kidogo. Sikumgusa hata kidogo, niliingia, amelala kwenye machela, bila shaka kulikuwa na wagonjwa wengine, bali nilihusika juu ya mtoto huyo, kushika roho yake nilipozungumza naye. Naye alionekana kama, msichana mdogo mzuri sana, sioni kwa nini mtoto huyo alijaze kaburi kabla ya wakati wake, na hiyo haina budi kuwa ni ibilisi akijaribu kuuchukua uhai wake. Kwa hiyo kamwe sikumgusa huyo mtoto hata kidogo, nikaenda moja kwa moja mimbarani pamoja na Neno, na kudumu moja kwa moja na Neno, nalo Neno likamponya kwa ghafla sana mpaka akasimama na kuondoka, ni mzima sasa, naye anaishi kama mtu mwingine yeyote, huwezi kupata dalili yake popote. Hata sikuligusa Neno, ama, kumgusa yeye.

20 Mnaona, Neno lilitoka, naye akaliamini Neno, nalo Neno ni Uzima wa Mungu na Nguvu za Mungu, nalo Neno ndilo linalolifanya, Neno huwaponya wagonjwa.

Ndipo mnasema, "Vema, Yesu aliwaponya wagonjwa."

21 Yeye ni Neno, Yeye ni Neno, na unapolipokea Neno, unampokea Yesu, kwa kuwa Yeye ni Neno, "Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Tunaamini hilo, sivyo? Kila sehemu. Tunaamini ya kwamba Kristo ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, nasi tunaamini ya kwamba Bibi-arusi Wake hana budi kuwa ni kitu kile kile. Tunaamini ya kwamba hana budi kuamini kila sehemu ya Neno na awe na Neno hilo ndani Yake, kwa sababu Yeye ni sehemu ya ule Mwili, Yeye ni Mwili ambapo Yeye ni Kichwa.

22 Na wakati alipokufa, na kufufuka katika wafu, na kufufuka, na kuketi huko Juu kwenye, karibu na ukuu wa Mungu kwenye Kiti Chake cha Enzi, mkono wa kuume wa Ukuu, basi, nasi ni wajumbe Wake, nasi tunajihesabu kuwa tumekufa, na kuzikwa kwa ubatizo, tukafufuka pamoja Naye, na sasa tumeketi pamoja, pamoja Naye, katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Hilo lingetufanya sote kupaza sauti, sivyo? Wazia hilo: Sisi ni, si, "tutakuwa," ndivyo tulivyo *sasa*. *Sasa* sisi ni wana wa Mungu, *sasa* sisi ni binti za Mungu. Sio, "tutaketi," *sasa* tumeketi. Hatuwezi . . . ninii . . .

23 Yesu alisema Maandiko hayana budi kutimizwa. Kila Neno halina budi kutimia. Siku hizi tumeliacha kwa mbali sana, tumejichanganyisha tu na kanuni za imani na kadhalika, mpaka tumeshikwa na ha—hamaki kali, kama tu vile Biblia ilivyosema tungefanya, hasa.

24 Adamu, kabla hajamfikia mkewe, alitiwa mimba ya mbegu mbaya. Alichukua uongo wa ibilisi na kujaribu kuuchanganya na Neno la Mungu, nao ukasababisha mauti. Mtoto wa kwanza aliyezaliwa kutoka kwake alikuwa na mauti, kila mtoto tangu hapo amekuwa na mauti.

25 Mke wa Yehova, wakati alipompandisha kutoka Misri na kumtakasa na kumwingiza barabarani, alifanya nini? Alifanya jambo lile lile. Yehova alimpeleka mke Wake kwenye nchi ya ahadi, akienda zake kule juu alimsikiliza nabii wa uongo jina lake Balaamu, naye alifanya nini? "Mbona, hakuna tofauti kati yetu, hebu sote tuungane pamoja, na tuwe familia moja."

26 Hivyo ndivyo bibi-arusi amefanya na ulimwengu, ameungana na ulimwengu pamoja na kanuni zake za imani na kadhalika, na kulikana Neno la Mungu, akisema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu." Naye yuko wapi sasa? Ametalikiwa. Ninii tu... bibi-arusi wa Yesu alikuwa amefanya jambo lile lile ambalo bibi-arusi wa Yehova alifanya, na jambo lile lile ambalo—ambalo bibi-arusi wa Adamu alifanya. Naam, lile lile hasa. Biblia ilisema, "Kinywa cha mashahidi watatu na lithibitike kila neno." Kuna makanisa matatu, bibi-arusi watatu, wote walifanya jambo lile lile.

27 Lakini mbele ya hayo yote, kunaye Bibi-arusi halisi ambaye Mungu anamleta, naye ana sehemu ndogo kutoka kwa kila... Kila wakati kumekuwa na matengenezo, kumekuwa na *kiasi fulani* cha Neno lililoenezwa, na kila kizazi hupata wakati wake. Mliwahi kuona? Kutakuwako na mtu wa Mungu atakayekuja ambaye atawasha moto pamoja na Mungu, na kutakuwa na uamsho mkuu utakaoenea nchini. Basi ni jambo gani linalotukia? Mara baada ya hayo wanachukua wazo la mtu huyo, na kuliundia dhehebu, na kuingiza kanuni za imani, na kujichanganyisha nayo. Hapo linakufa wala halifufuki tena, hiyo ni kweli, daima imekuwa, daima itakuwa, kila wakati.

28 Lakini kila kizazi, kinapata nini? Nafasi yake kwenye Neno jipya la Mungu kila wakati, kama vile Luther chini ya kuhesabiwa haki, kama vile Wesley chini ya utakaso, huduma ya Kipentekoste chini ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mnaona? Kila mmoja anapata nafasi yake. Basi watu wanaowafuata hao watengenezaji wakuu wanafanya nini? Wanaliundia dhehebu, wanaliundia shirika, wanalichanganyisha na kanuni za imani, kidogo *hapa* na kidogo *pale*. Kundi jipya la wasomi wa shule linakuja pamoja na lundo la saikolojia, kama tu vile Hawa alivyokuwa akijaribu kupata nuru mpya, kuichanganya na Neno la Mungu, mauti, madhehebu yakaondoka, yakafa kiroho. Hiyo ni kweli kabisa, hivyo ndivyo imekuwa daima.

29 Sasa, amini usiamini, huenda usifikiri hivyo, lakini nitazungumza, usiku wa leo, Bwana akipenda, juu ya somo la *Ishara Mbegu Ya Wakati Wa Mwisho*. Ishara Mbegu itakuwa ni ishara ya namna gani wakati wa mwisho? Kabla hatujasoma Neno, hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza na Mwandishi Wake.

30 Sijui, usiku wa leo, huku vichwa vyetu vimeinamishwa,

tukitambua ya kwamba tunaishi katika vivuli vya kuja kwa Mwana wa Mungu, sijui kama kunaweza kuwako haja, usiku wa leo, ungetaka kumjulisha Mungu kwamba wewe ni mwaminifu, nawe una jambo fulani moyoni mwako ambalo unataka Mungu akutendee? Mwinulie tu mikono yako, useme, “Huyu ni mimi, Mungu, ninataka *hiki* na *hiki*.” Asanteni.

31 Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia Kiti Chako cha Enzi cha neema, kamwe si Kiti Chako cha Enzi cha Hukumu. Mungu, hatutaki Hukumu, kwa sababu tusingeweza kusimama kwenye Kiti hicho cha Enzi, bali tuna furaha sana ya kwamba kulikuwa na Mtu aliyesimama pale kwa ajili yetu, Mwanao, Bwana Yesu. Yeye alisimama pale kwa ajili yetu, na kuzistahimili Hukumu, tupate kuwa na haki ya kukikaribia Kiti cha Enzi cha neema, nasi tunakaribia, usiku wa leo, katika Jina Lake.

32 Naye alisema Mwenyewe, na kila Neno lililotoka Kwake lilikuwa ni Maandiko, na hayana budi kutimizwa, Yeye alisema, “Mkimwomba Baba Yangu neno lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Sasa, tunajua ya kwamba Neno hilo ni kweli, nasi tunakaribia, katika Jina la Yesu, kumwomba Baba yetu wa Mbinguni atujalie neema ya msamaha kutoka kwenye Kiti Chake cha Enzi cha neema chenye upendo.

33 Tunamwomba, usiku wa leo, alidhihirishe Neno Lake kwetu, na kutufunulia saa tunayokaribia, kwa maana hatutaki kujikwaa kama watu tusiojua tunakoelekea. Mtu asiyejua aendako, hujikwaa. Nawe ulisema tulikuwa watoto wa Nuru, nasi tunapaswa kujua tunakoenda, hatua kwa hatua, kama walio na taa, inaonyesha, si kote chini, bali tunapopiga hatua. Ninaomba, Baba, tunapopiga hatua hii usiku wa leo, kuelekea mkutano huu, kwamba tutaona kilicho kusudi la Mungu kwetu kuwa hapa.

34 Nami nakuomba Wewe, Ee Bwana, ya kwamba kila mkono ulioinuliwa kwenye mkutano huu usiku wa leo, utakuwa, kusudi la haja hiyo nyuma ya huo mkono, lijibiwe. Kama ni kwa ajili ya wokovu, Mungu, tujalie usiku wa leo, kwamba wataupokea. Kama ni shida ya nyumbani, yanyoshe hayo makazi, Bwana, tupe amani. Kama ni kwa ajili ya mtu anayedhikika, mpe rehema Yako, Baba. Kama ni kwa ajili ya mtu mgonjwa, jalia Maneno ya uponyaji wa Mungu yapenye ndani kabisa moyomi mwao usiku wa leo, ambayo yataleta zao la afya njema ya Kiungu kesho. Tujalie, Bwana, utusikie.

35 Tunaliwasilisha Neno kwako, usiku wa leo, pamoja nasi wenyewe na mafungu haya, upate muktadha kutoka Kwake, na kutufunulia mambo tunayopaswa kujua. Wabariki watu hawa, ibariki shule hii. Katika siku hizi ambapo mtu angesema watafanya mkutano, kundi lisilo la kimadhehebu, wangaliikatalia bila huruma, lakini huyu mkuu wa shule aliufungua mlango. Tunaomba, Mungu, ya kwamba Wewe

utambariki, na kumjulisha ya kwamba imeandikwa katika Maandiko, “Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hawa walio wadogo, mlinitendea Mimi.”

“Ni lini ulipokuwa mhitaji, nasi hatukuhudumu?”

Nawe ukasema, “Nitasema, ‘Kadiri mlivyowatendea hawa, mmenitendea Mimi.’”

Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba kutoka kwenye shule hii watatokea wahubiri wenye nguvu, waliotiwa mafuta kwa ajili ya siku zijazo.

36 Ninamwombea kila mtu aliye hapa, wachungaji wao, yabariki makanisa yao, Bwana. Jalia huo uamsho mkuu utokee katika hii jamii hapa miongoni mwa watu, na kuwafanya wengi waokolewe. Waponye wagonjwa na wanaoteseka, jipatie Mwenyewe utukufu. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

37 Maskini usomaji wa kigeni sana wa Maandiko, mtakapoenda nyumbani ningetaka msome mlango huo, Amosi mlango wa 3 na kifungu cha 7. Mazingira ya kipekee kwa ajili ya somo, lakini mwajua, Mungu hufanya mambo ya kipekee na yasiyo ya kawaida, hufanya kazi kwa njia za kipekee, njia za ajabu, kufanya maajabu Yake. Amosi 3:7:

> *Hakika Bwana* MUNGU *hatafanya neno lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake.*

38 Sasa, somo ambalo ningetaka kutumia ni hili: *Ishara Mbegu Ya Wakati Wa Mwisho*. Na kama vile ndio kwanza niwaambie jana, nikihubiri sana juu ya Mbegu kwa kuwa Hiyo ni Neno, vitu vyote vilianzia katika Mwanzo, maana *Mwanzo* maana yake ni “chanzo,” ama “mlango wa mbegu ya Biblia.” Kila kitu tulicho nacho duniani leo hii, asili yake ilianza katika Mwanzo.

39 Sasa, tuna vitu siku hizi ambavyo havikuanzia katika Mwanzo, kwa sababu vimefanyizwa kichotara. Chochote chotara ni bandia, hakifai, hakiwezi kujizaa chenyewe. Chochote kilicho chotara ni cha kujibunia, wala hakiwezi kujirudisha tena.

40 Kama nilivyosema mara nyingi, hebu tuchukue uzalishaji mifugo, kama vile unavyomchukua pu—punda na farasi jike, nao wanazaa nyumbu, lakini nyumbu hawezi kujizaa tena. Hajui baba wala mama ni nini, amechanganyikiwa.

41 Hebu tuchukue mahindi siku hizi, ni chotara, wao wanasema, “Yana masuke mazuri zaidi, makubwa zaidi,” bali hayafai kitu. Mnaona yale *Reader’s Digest* iliyoandika hivi punde juu yake? Kama wanawake wakiendelea kula kuku na nyama ya ng’ombe na kadhalika ambazo ni chotara, katika miaka ishirini tangu sasa jamii ya binadamu itakwisha, wanawake hawawezi tena kuzaa watoto. Hiyo ni kweli. Kuchanganya mbegu, hakufai kitu.

42 Chukua mahindi, yazalishe kwa kuchanganya mbegu, yanazaa suke kubwa mno. Yanafanya nini? Vema, ukitaka kuyala kwenye suke kubwa. Lakini inakuwaje kwake? Yapande tena, hayawezi kujizaa tena, hayafai kitu, yamekufa. Kwa hiyo, chochote ambacho hakikunenwa na Mungu hapo mwanzo ni chotara.

43 Na hivyo ndivyo watu wanavyoliacha Neno la Mungu. Linakuwa ni jambo la kichotara, halina budi kufa, haliwezi kuzaa Uhai wa aina yake tena. Kanisa litakalokataa ku—kuliamini Neno la Mungu ni kanisa chotara pamoja na mafundisho ya sharti, kanuni za imani, mafundisho ambayo si ya Kimaandiko. Kanisa hilo haliwezi kumzaa mtoto aliyejazwa na Roho maana ni chotara, halifai kitu. Huenda likawa ni kuta kubwa zaidi, mabenchi mazuri, kengele kubwa, viti vya kifahari, lakini hilo halimaanishi kitu, limekufa kiroho. Hiyo ni kweli. Haliwezi kuzaa watoto waliojazwa na Roho, kwa sababu lenyewe limekufa.

44 Sasa, nikizungumza kwa saa sita juu ya somo hilo, na usiku wa leo, nikirudi tena kwenye hii hii *Mbegu Ishara Ya Wakati Wa Mwisho*. Sasa, watu wote wenye hekima, kama yeye ana akili timamu, daima anajaribu kuona kilicho mbele yake, sisi sote tunataka kujua hilo. "Nitapiga hatua gani tena? Niende wapi kutoka hapa?" Ni kama mtu anayevuka kijito, anakanyaga jiwe moja, ndipo anaangalia pande zote aone hatua yake ya pili itakuwa wapi, kwa kuwa asipofanya hivyo, kamwe hawezi kuruka tu popote, akiruka atajizamisha mwenyewe, hana budi kuangalia anakoenda, "Nikiisha kuuvuka *huu*, wapi basi?" Sisi sote tuko hivyo, hicho kimekuwa ndicho kilio cha jamii ya binadamu kote katika nyakati, "Wapi kutoka hapa?"

45 Mfalme wa Uingereza, usiku mmoja, wakati mtakatifu mmoja alipombatiza, kesho yake asubuhi, walikuwa wakiota moto, mkubwa mno, kama barazani, basi kulikuwa na tanuru kubwa la moto, ama tungeiita chanja ya chuma, ni mahali tu pakubwa, pakubwa mno, ambapo palikuwa pamewekwa magogo. Huyo mtakatifu alikuwa akijaribu kumwambia huyo mfalme habari za Mungu, ndipo maskini shorewanda akayamaliza mahubiri yake. Maskini shorewanda, usiku, aliruka gizani, akaingia kwenye nuru, akarudi kutoka kwenye nuru, akaingia gizani, ndipo huyo mtakatifu akasimama, akamwambia mfalme, "Je, alitoka wapi, na alienda wapi?"

46 Hilo ndilo tunalotaka kujua, "Tulitoka wapi?" na, "Tunafanya nini hapa?" na, "Tunaenda wapi kutoka hapa?" Sasa, wao, sayansi yote tuliyo nayo, kadiri tulivyochimbua mifupa mingi, kadiri tulivyoandika vitabu vingi, hakuna hata kitabu kimoja kinachoweza kukwambia unakotoka, kile ulicho, na mahali unapoelekea, Kitabu kimoja tu, na hicho ni Biblia. Inakwambia unakotoka, kwa nini uko hapa, na unakoenda. Kwa

hiyo basi, kama tunataka kujua "Ni wapi kutoka hapa?" hebu tuchukue Kitabu pekee kinachoweza kutuambia.

47 Mifupa ya kale wanayochimbua, na—na stalagmiti, na kadhalika, haiwezi kuthibitisha chochote. Neno la Mungu lina jibu, lina jibu la kila kitu tunachouliza, kiko katika Kitabu cha Mungu. Mwanadamu mara nyingi ameshangaa, tunashuka wakati mwingine, na kusoma Maandiko, na kushangaa kuyahusu, bali hatupaswi kushangaa, huwezi kuyaelezea, huna budi kuyaamini.

48 Hakuna mtu awezaye—awezaye kumthibitisha Mungu kisayansi. Kama ungeweza kumthibitisha Mungu, kisayansi, basi si imani tena. Tunapaswa kumwamini Mungu, na imani si ya kisayansi.

49 Vipi kama Musa angalivuta baadhi ya hayo majani kutoka kwenye ile miti na kusema, "Ninaamini nitayapeleka kwenye maabara nione ni kemikali gani iliyo juu yake ambayo inaizuia kuteketea"? Mnaona, Mungu kamwe asingezungumza naye. Hakujua hilo, jambo pekee alilofanya lilikuwa ni kuvua viatu vyake na kuketi chini kwa uchaji, ndipo Mungu akamjibu.

50 Hatuwezi kuthibitisha ahadi hizi za Mungu kisayansi, bali tunaangalia nyuma na kuona ambapo, katika majira yake, kila moja ya hayo yalitukia jinsi tu Mungu alivyosema yangetukia. Kwa hiyo kwa uchaji na heshima kwa Neno Lake usiku wa leo, hebu na tuketi tu chini kwa kitambo kidogo na kuliangalia, ndipo tuone tunakoelekea, kusudi lake ni nini. Tuko hapa kwa sababu gani? Yote yanahusu nini?

51 Hapa wakati fulani uliopita nilikuwa huko magharibi, nami nilikuwa nimesimama katika nyumba ya mtu aliyenialika hulo nje kwa—kwa chakula cha kutwa, naye akasema, "Bw. Branham, ninakuona ukivutiwa na huo mchongo, mchoro," ama, si mchoro, lakini kidogo ilikuwa imechongwa kwa mbao, kitu kama ubao, juu mekoni.

52 Nikasema, "Naam, Bwana, naam." Nayo ilikuwa ni kigari cha kale cha maksai, ama, mkokoteni uliofunikwa pamoja na maksai, mtu mmoja mbele, mvulana mdogo ameketi kitini pamoja na mama yake, nao walikuwa wakisafiri.

53 Naye akasema, "Huyo alikuwa ni baba na mama yangu, naye huyo mvulana mdogo kitini alikuwa ni mimi mwenyewe." Akasema, "Tulikuja hapa katika mkokoteni huu wa maksai," akasema, "lakini tangu wakati huo, tumefanikiwa *sana*." Akasema, "Nataka uje hapa nje uani." Akasema, ninasahau ni maelfu mangapi ya ekari alizomiliki kule za ranchi, akasema, "Nilinunua hizo katika siku za ujana wangu." Kisha akasema, "Kisha baada ya hizo, ranchi inayopakana nayo magharibi, ninaimiliki; ranchi inayopakana nayo upande wa kusini, ninaimiliki." Kasema, "Unauona ule moshi kule?"

"Naam, Bwana."

Kasema, “Huo ni mji.” Ninasahau ni mali kiasi gani alimiliki kule.

Akasema, “Mimi ndiye rais katika benki ile kule,” akiniambia yote aliyomiliki.

54 Nikasikiliza kwa muda kidogo, kisha nikasema, “Ningetaka kukuuliza swali moja, Bwana. Umeelekeza upande wa mashariki, na magharibi, ukionyesha ranchi, na kwenye ule mji, ningetaka uangalie juu upande *huu*, uone, kisha uniambie unamiliki kiasi gani *huko* juu.” Hilo ndilo jambo muhimu, kwa sababu siku moja utaacha kila kimoja cha haya hapa chini, ndipo basi, utaenda wapi kutoka hapo? Hilo ndilo jambo muhimu.

55 Huku ni kukaa hapa muda mfupi, bali huko ni kukaa Milele Kule. Kwa hiyo nafikiri tunapaswa kufikiria mahali tunakoelekea kwa Umilele. Kama tunaweza kushughulikia, na kuzitunza familia zetu, na kadhalika hapa duniani kwa makazi, nyumba, na starehe, hiyo, elimu, hayo ndiyo mambo tunayopaswa kufanya, lakini ninii, moja ya mambo muhimu tunayopaswa kufanya, hatulishughulikii mpaka tutakapofikia mwisho wa safari, na kujizamisha katika Umilele, bila kujua chochote kumhusu Mungu, kuhusu mpango Wake wa wokovu, na neema ya ukombozi ya Yesu Kristo. Inasikitisha kwamba tunafanya hivyo, lakini tunafanya hivyo.

56 Watu wenye hekima, wanapoona kwamba wao ni kiumbe cha wakati, wanashangaa kuna nini baada ya wakati kwisha. Sasa nitazungumza juu ya mtu jina lake Ayubu kwa dakika chache; hicho ndicho Kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia. Tunafahamu ya kwamba Ayubu alikuwa mmoja wa watu wenye hekima sana katika ulimwengu wa siku zake. Mbona, alisema wakati akienda sokoni hao watawala vijana wangesujudu mbele zake wapate hekima.

57 Alikuwa ni mtu mashuhuri, lakini mtu huyo akaanza kutambua, juu ya ukuu wake wote, alishangaa ni nini, baada ya haya yote kwisha, basi kutakuwa na nini? Alishangaa ni nini kitakachotukia. Kwa hiyo anazungumza basi, na kuanza kuuchunguza uumbaji wa Mungu, alijua ya kwamba vitu vyote viliumbwa kwa Neno kutoka kwa Mungu. Nasi. . .aliona pia, akasema, “Kuna matumaini mti ukifa, utaishi tena.”

58 Ukiangalia maumbile, Mungu, katika njia Yake kuu ya kuonyesha hisia Zake kwa watu wapate kuwa na hakika, kama wana Biblia ama chochote kile, Yeye hujidhihirisha Mwenyewe katika maumbile kwako. Angalia jua linapochomoza asubuhi. Inakuwaje kwa jua? Ni mtoto mchanga, aliyezaliwa mashariki, yapata saa nne liko katika ujana wake, adhuhuri liko katika nguvu zake, alasiri liko kwenye umri wake wa makamu, na jioni limetoweka, linatua, limekwisha. Je, huo ndio mwisho wa jua? La. Mungu ana kusudi kwa ajili ya jua, kwa hiyo jua hurudi

na kuchomoza tena kesho yake asubuhi. Linanena juu ya nini? Kuzaliwa, maisha, mauti, kufufuka.

59 Angalieni maua yenu, nilikuwa nikiona leo hii, nikishuka huku, maua, jinsi yalivyo mazuri. Yako hapa kwa kusudi fulani, hayo ni Maneno ya Mungu yaliyonenwa. Mungu aliyanena yakawepo, na wakati alipoyanena, angalieni kinachotukia: Yanapendeza yakisimama uani mwako, baada ya kitambo kidogo, jalidi inayapiga, madogo, makubwa, ya umri wa kati, mara ikiyapiga ni mauti. Yanainamisha maskini kichwa chao, ndipo inakuwaje? Mbegu ndogo nyeusi ya namna fulani inaanguka kutoka kwayo. Amini usiamini, Mungu ana msafara wa mazishi kwa hayo. Mvua ya masika inakuja pamoja na machozi, tuseme, yanashuka kutoka angani na kuizika hiyo mbegu.

60 Majira ya kipupwe yanakuja, petali zimekwisha, ubua umekwisha, tunguu limekwisha, hiyo mbegu inaganda, inapasuka, nyama inatoka. Huo ndio mwisho wa hiyo mbegu? La, bwana. Hebu jua hilo lenye joto liangaze, ambalo linaleta ufufuo wa uhai wote wa mimea, mara jua hilo linapoanza kuangazia dunia na kupata joto, kuna chembe ya uhai mahali fulani katika mbegu hiyo, nayo inaishi tena. Kwa nini? Ilitimiza kusudi la Mungu, naye Mungu anaifanyia njia ipate kuishi tena.

61 Sasa, tuliwekwa hapa kwa kusudi fulani, bali hatuna budi kulitumikia kusudi hilo, tuchague ama mauti au Uzima. Kwa hiyo tumewekwa hapa kwa kusudi fulani, bali hatuna budi kulitumikia kusudi hilo, huko ni kumtumikia Mungu, kwa sababu sisi ni wana na binti za Mungu.

62 Sasa, Ayubu aliangalia uumbaji, aliona ya kwamba baada ya mauti hayakuwa ndiyo mwisho wake, aliona ya kwamba baada ya mauti kulikuwa na uhai tena. Uhai, mara jua lilipokuwa sawa, ilikuwa ni uhai tena. "Vema," akasema, "kama mbegu hiyo ni mbegu iliyonenwa, ama Neno la Mungu lililonenwa, nayo inatimiza kusudi lake kisha inakufa . . . Lakini," akasema, "mtu . . ." Ninaangalia Maandiko fulani hapa kutoka kwa Ayubu sasa, Ayubu 14, "Lakini mwanadamu analala chini, hutoa roho, huifariki dunia. Wanawe wanakuja kuomboleza, yeye hajui. Yuko wapi? Laiti ungenificha kuzimuni, na kuniweka mahali pa siri, hata ghadhabu Zako zitakapopita!"

Ayubu alisema, "Ninaona ua likifa, linatimiza kusudi lake, kisha linafufuka. Ninaona mti ukifa, majira ya kupukutika mwakani yanachanua majani yake."

63 Mliwahi kuona mti? Utachanua jani lake, kisha litatimiza wakati wake katika msimu wa kiangazi, majira ya kupukutika yanakuja, *muda mrefu* kabla jalidi haijashuka, jani hilo linaanza kugeuka manjano, jekundu, kahawia, baada ya kitambo kidogo linapukutika kutoka mtini, linaanguka chini. Je, huo ndio mwisho wake? La. Ni kitu gani kinachotukia? Uhai uliokuwa

kwenye jani hilo unarudi kwenye shina la mti, mahali unapotoka. Unafanya nini basi? Majira ya kuchipua ya mwaka, unazaa, katika ufufuo, jani jipya, uhai ule ule, unarudi na jani jipya.

64 Nao Wakristo wananing'inia kwenye Mti wa Uzima, na uhai unapouacha mwili huu mwovu wenye dhambi, unarudi kwa Mungu anayeutoa, upate kurudi tena na ule mpya, kwa sababu unatumikia kusudi fulani.

65 Hapa wakati fulani uliopita nilikuwa huko chini katika jimbo la Kentucky, ama, nadhani kutoka hapa, kwa mwelekeo, ingenibidi kuelekeza kaskazini, huko *juu* katika jimbo la Kentucky, nilikuwa nikiwinda, mimi na Bw. Wood, mmoja wa wadhamini hapa pamoja nasi usiku wa leo. Nami nilikuwa nimefanya mkutano huko katika mji mdogo unaoitwa Acton, kwenye uwanja wa kambi wa Methodisti. Mle ndani kulikuwa na usiku mmoja tuliokuwa tukizungumza, naye Bwana alikuwa akifanya mambo makuu, nasi tulikuwa na ibada ya uponyaji, tukiwaombea wagonjwa. Ninyi nyote mliokuwa hapa kwenye ule mkutano mwingine, mnajua kinachotukia.

66 Nami siwezi kuponya, hakuna mtu mwingine, Mungu tayari amefanya hivyo, inakubidi tu kuamini. Kwa hiyo Yeye anayo njia, ambayo aliahidi katika siku za mwisho, karama ambayo ingezitambua roho, na kadhalika, zinazofanya kazi, tunajua hilo, asilimia mia moja, maana ni Neno la Mungu likidhihirisha ahadi Yake kwa ajili ya siku hii ya mwisho.

67 Na mle ndani, kulikuwa na mwanamke, sikuwa nimewahi kuwa kwenye hiyo nchi hapo awali, basi kulikuwa na mwanamke aliyeketi nyuma kwenye kusanyiko, ndipo Roho Mtakatifu akaingia miongoni mwa watu na kuanza kumwita *huyu*, *yule*, akiwaambia. Ilikuwa ni Bwana wetu Yesu, Neno Lake likidhihirishwa katika Mwili wa Kanisa Lake. Ndipo basi alipoanza kunena, Yesu alisimama mahali hapo, akiyajua mawazo ya mioyo yao, akaongea nao, akawaambia watu juu ya mambo mbalimbali, kama ninyi nyote wasomaji wa Biblia mjuavyo, aliahidi jambo lile lile tena kurudia katika siku za mwisho, aliahidi hilo kwa Maandiko Yake kwamba litafanya hivyo.

68 Sasa, nawatakeni mwone, sasa, wakati hilo lilipokuwa likitukia, huko nyuma kabisa mama mmoja alikuwa akilia, mahali fulani kwenye uwanja mkubwa wa kambi, mamia na mamia mengi mengi ya watu walikuwa wameketi, na kulikuwako na mama aliyekuwa akilia. Angalieni, Roho Mtakatifu akamwendea huyo mama na kusema, "Unamlilia dada yako, jina lake ni *Fulani-wa-fulani*, anaishi mahali fulani. Una leso kwenye pochi yako uliyoweka mle kabla ya kuondoka nyumbani. Ni leso iliyo *hivi-na-hivi*. Wewe chukua leso hii uende

ukaiweke juu ya dada yako, yuafa kwa kansa, na BWANA ASEMA HIVI, ataishi.”

Huyo mwanamke akaondoka humo jengoni, akaenda na kuweka leso yake juu ya mama huyo usiku huo, na kesho yake asubuhi alikuwa mzima.

69 Sasa, kwa hiyo nilikuwa (Huo msimu ulikuwa na joto sana.), nikiwinda kuchakulo. Kama vile wengi wa wawindaji kuchakulo wenzangu wajuavyo, wao ni . . . wao . . . kuchacharika kwa majani huwaogopesha kuchakulo, nasi, kulikuwa kukavu sana, ilitubidi kwenda mahali ambapo palikuwa na mabonde ambayo tungeweza kuingia, mitaro midogo, kutembea kupitia mwituni. Jina la rafiki yangu lilikuwa ni Bw. Wood, ameketi hapa mkono wangu wa kuume.

70 Basi akasema, “Ninamjua mtu ambaye ana shamba la ekari nyingi. Lakini,” kasema, “ni mgumu sana.” Kasema, “Yeye ni kafiri,” kisha kasema, “hamwamini Mungu,” naye akasema, “yeye, analidhihaki.” Naye akasema, “Lakini ananijua, anamjua baba yangu.” Naye akasema, “Kama nikienda kumwuliza kama tunaweza kuwinda katika eneo lake . . . ”

Nikasema, “Hebu twende.”

71 Tukaendesha gari huko nyuma kabisa mashambani, huko nyuma kabisa kwenye barabara ya kando, basi wazee wawili walikuwa wameketi chini ya kivuli cha mtofaa, akasema, “Yule pale, yule aliye upande wa kulia.”

Nikasema, “Kwa kuwa mimi ni mhudumu, afadhali niketi kwenye gari.”

Kwa hiyo akatoka nje, na kusema, “U hali gani?”

Ndipo huyo mtu akasema, “Karibu huku, keti chini.”

Akasema, “Jina langu ni Wood,” akasema, “sijui kama ungejali kama tungewinda kidogo huku kwako.”

Akasema, “Wewe ni Wood yupi?”

Akasema, “Mimi ni mwana wa Jim Wood.”

Akasema, “Jim Wood ni rafiki yangu, na yeyote wa watoto wake anaweza kuwinda popote watakapo.”

Kasema, “Asante.”

Kasema, “Nashangaa sasa,” akasema, “wewe ni yupi?”

Akasema, “Mimi ni Banks.” Akazungumza naye dakika chache, ndipo Bw. Wood akasema, “Sijui kama ingekuwa sawa kwangu kwenda pamoja na mchungaji wangu.”

Akasema, “Usiseme umekuwa duni sana hata inakubidi kubebana na mhubiri popote uendapo?”

Akasema, “Mchungaji wangu yuko pale nje.”

Nikawaza, “Afadhali nitoke kwenye gari.” Ndipo nikatoka kwenye gari, nikaenda pale, na kusema, “Jambo?”

Akasema, “Jambo? Wewe ni mhubiri ati?”

Nikasema, “Naam, Bwana.”

Naye akasema, “Vema,” akasema, “inasemekana mimi ni kafiri.”

Nikasema, “Vema, hamna mengi ya kujivunia, sivyo?”

Akasema, “Nadhani sivyo.” Akasema, “Lakini mimi, kile nilicho nacho dhidi yenu enyi watu, mnazungumza juu ya Kitu msichokijua.”

“Loo,” nikasema, “hiyo ni kweli?”

Akasema, “Naam, Bwana, daima ninawasikia wakivumisha kuhusu jambo *hili*, kuhusu Mungu fulani, na kila kitu,” kasema, “hakuna Kitu kama hicho.”

72 Nikasema, “Um-hum.” Nikasema, “Vema, bila shaka unajua jinsi ilivyo, Bwana,” nikasema, “kila mtu na wazo lake mwenyewe.” Nilikuwa nikiwazia moyoni mwangu, “Sasa, Bwana, Wewe nipe kitu cha kumsaidia mtu huyo, bila shaka ni mwaminifu.”

Naye akasema, “Nimemwona mhubiri mmoja tu maishani mwangu mwote ni—ningependa kusikia, kusikia habari zake.”

Nami nikasema, “Huyo alikuwa ni nani, Bwana?”

73 Akasema, “Hapa yapata miaka miwili iliyopita, kulikuwa na mhubiri hapa kwenye mji uitwao Acton.” Akasema, “Na maskini bibi *Nanii*, hapa juu kilimani, alikuwa amelala pale kwa miaka miwili akiwa na kansa.” Kasema, “Mimi na mke wangu, wasingeweza kumweka kwenye maliwato ya kitandani tena, iliwabidi kutumia shuka la kuvutwa,” kisha kasema, “tulikuwa huko juu asubuhi hiyo,” tena kasema, “daktari alikuwa amesema hivi majuzi kwamba asingeishi usiku kucha.

74 “Alikuwa na kansa tumboni mwake, alikuwa ameliwa. Hata asingeweza kunywa maji ya shayiri, wala hakuwa ameyanywa kwa majuma kadhaa, walikuwa wamemlisha glukosi kupitia mishipa yake, mpaka mishipa yake ikakunjana.” Kisha kasema, “Hakuna kitu angaliweza kufanyiwa.”

75 Kisha kasema, “Dada yake alikuwa ameketi hapo akimsikiliza mhubiri huyo akihubiri, naye mhubiri huyo hakumjua mtu yeyote huku, hakuwa amewahi kuwa huku, naye akamwambia yeye alikuwa ni nani, na dada yake alikuwa ni nani, kisha akanena kuhusu leso aliyokuwa nayo, na kusema, ‘Iweke juu ya mwanamke huyo.’” Kisha kasema, “Usiku huo nilifikiri walikuwa na Jeshi la Wokovu huko juu mahali fulani, makelele hayo yote.” Kisha kasema, “Kesho yake asubuhi tukaenda huko kuona kama alikuwa amekufa.” Ndipo kasema, “Tulipofika kule alikuwa ameamka, akipika sambusa za matofaa ya kukaangwa na kuyala.” Kisha kasema, “Hata hufanya kazi ya jirani.” Akasema, “Sasa . . . ”

Nikasema, “Kwani cha ajabu hapo ni kipi?”

76 Akasema, “Vema, hili ndilo ninalotaka kujua, kama nikiwahi kumwona mhubiri huyo, nitamwuliza, ni kitu gani kilichomwambia kuhusu mwanamke huyo, na kama angeponywa.”

77 “Loo,” nikasema, “naam, Bwana.” Damu ya kuchakulo kote mwilini mwangu, na masharubu machafu, yapata urefu *huo*, mwajua, nami nikasema, “Sionekani sana kama mhubiri sasa.”

Akasema, “Vema, inaonekana ya kiutu zaidi.”

Nami nikasema, “Naam, Bwana.” Kwa hiyo, nikasema, “Naweza kula moja ya hayo matofaa?” Maskini manyigu walikuwa wameyavamia kabisa.

Naye akasema, “Naam.” Nikaokota moja, nami nikaliuma. Naye akasema, “Jihudumie, manyigu wanayala.”

Nami nikasema, “Asante.” Basi nikaliuma, nikasema, “Hilo ni tofaa zuri.”

Akasema, “Naam,” akasema, “mti huo wa kale umenizalia mengi.”

Nami nikasema, “Naam, Bwana.” Nikasema, “Huo mti una umri gani?”

Akasema, “Karibu umri wa miaka arobaini.” Kasema, “Niliupanda pale, tawi tu.”

Nami nikasema, “Uh-huh.” Nikasema, “Ninaona matofaa yote yanaanguka kutoka kwake, nayo majani yanapukutika.”

Akasema, “Naam, hivyo ndivyo yafanyavyo.”

Kisha nikasema, “Ninataka kukuuliza swali.”

Kasema, “Naam, Bwana, endelea ukaulize.” Akasema . . .

78 Nikasema, “Ni kitu gani kinachosababisha . . . ? Sasa, hatujawa na jalidi,” nikasema, “ni katikati tu ya Agosti, hatutakuwa na jalidi mpaka Oktoba au Novemba,” nikasema, “lakini hapa, katikati ya Agosti, hayo majani yanapukutika mtini.” Nikasema, “Ni kitu gani kinachoyafanya hayo majani kupukutika?”

“Vema,” akasema, “utomvu unaondoka.”

Nikasema, “Vipi kama huo utomvu hautaondoka?”

79 Akasema, “Mbona, ungeninii, huo mti ungekufa kwenye msimu wa baridi kali, chembe ya uhai iko kwenye huo utomvu.” Akasema, “Kama ungeninii . . . Ingeuua huo mti, ungekufa.”

80 Nikasema, “Naam, Bwana.” Nikasema, “Kwa hiyo huo utomvu unarudi chini kwenye mizizi ambako kuna joto, unakaa mle majira yote ya baridi kali, kisha unarudi tena wakati wa kiangazi, ukileta majani mengi zaidi na matofaa zaidi.”

Kasema, “Jambo ndilo hilo.”

81 Nikasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani." Nikasema, "Ni Akili gani, sasa, mti huo hauna yoyote, ni Akili gani inayoambia mti huo, 'Wakati wa baridi kali unakuja, shuka chini kwenye mzizi na ukae mle mpaka kwenye majira ya kuchipua mwakani'?" Nikasema, "Hebu tia maji kwenye ndoo, na uyaweke juu ya nguzo, uone kama yatashuka chini majira ya kupukutika mwakani yajapo. Hayatafanya hivyo." Nikasema, "Huna budi kukubali kuna namna fulani ya Akili inayoufanya utomvu huo uondoke mtini na kushuka mizizini; usipofanya hivyo, unakufa, hujificha upate kuulinda uhai wake. Sasa, huo mti hauna akili, kuna kanuni ya Mungu inayofanya hivyo."

Naye akasema, "Vema, kamwe sikuliwazia namna hiyo."

82 Nikasema, "Bwana, Akili ile ile inayouambia ule mti kule juu, utomvu kwenye mti huo ushuke mizizini, Akili iyo hiyo ndiyo iliyoniambia mwanamke huyo alikuwa ni nani, na kumwambia kitakachotukia."

Akasema, "Wewe siye yule mhubiri!"

83 Nikasema, "Naam, Bwana." Na hapo akaongozwa kwa Kristo, naye akafa Mkristo mwaka mmoja baadaye, yapata umri wa miaka themanini na mitano. Mnaona, Mungu yuko kote kutuzunguka, Mungu yuko kila mahali, na kama tutaangalia maumbile, tutamwona hapo.

84 Sasa, baada ya Ayubu kumpata katika mauti, kuzikwa, na kufufuka kwa maumbile, yakijizaa tena kwa jinsi yake, basi asingeweza kuelewa kilichompata mwanadamu, "Kama mtu," yeye anasema, "akilala chini, anatoa roho yake. Yuko wapi?" Sasa, mnaona, huo mti kamwe haukutenda dhambi, maumbile hayakutenda dhambi, mwanadamu alitenda dhambi. Kwa hiyo asingeweza . . .

85 Ndipo akiwa nabii, sasa, Biblia, somo langu, lilisema, "Yeye huwajulisha manabii Wake siri Zake," Neno la Bwana humjia nabii, na kwa kuwa ni nabii, tunajua hadithi ya Ayubu, hatimaye Mungu alimwelezea Ayubu, kwamba uzao wa mwanadamu haukuwa mkamilifu kwa sababu mama wa mwanadamu alikuwa ameshindwa kulitii Neno la Mungu. Alijaribu kulichanganya na kitu kingine, wala Neno la Mungu halitachanganyana na chochote. Hiyo ni kweli.

86 Yesu alisema, wakati alipokuwa hapa, "Ukiwa na imani kama mbegu ya haradali, ungeuambia mlima huu . . ." Kwa nini aliirejea mbegu ya haradali? Mbegu ya haradali haitachanganyisha mbegu, ni mbegu halisi ya haradali, haitazalishana na chochote. Basi akasema, vinginevyo, "Kama una imani kiasi hicho, Neno la Mungu, hilo halitachanganyana na kutokuamini, wala kulihoji . . ." Loo, ninajisikia wa kidini. Hilo hutalihoji!

87 Haidhuru ni hali gani ya mambo, na chochote kingine, hulihoji Neno la Mungu, unaliamini, unapaswa kuliamini. Laiti

Hawa angaliliamini tu, angalipokea, naye angezaa watoto vizuri, lakini kabla . . . mumewe hajamfikia, yeye . . . alimkuta tayari ametiwa unajisi, kama vile Yehova alivyofanya, na kama vile Yesu amefanya. Kulikuwa na unajisi katika tumbo la uzazi la mawazo yake, alikuwa ameikubali mbegu ya kutokuamini dhidi ya Neno la Mungu, kwa sababu ilizaa kitu fulani kwake angavu zaidi, naye alitaka maarifa zaidi.

88 Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Nimesimama kwenye shule, tungekuwa ni kundi la *wasio na elimu* kama si elimu, nayo elimu ni sehemu ya ustaarabu wetu. Lakini ustaarabu, elimu, huja tu kwa Ukristo. Ustaarabu ndio mashina ya Ukri- . . . ya, ama, Ukristo ndio mashina ya ustaarabu, kweli kabisa. Ustaarabu ulikuja kwa njia ya Kristo, bila shaka.

89 Sasa, kutokuliamini Neno la Mungu, ama kulichanganya na kitu fulani upate Nuru zaidi, huwezi kulichanganya, halitachanganyikana. Huna budi kuliamini jinsi tu Mungu alivyoliandika, na jinsi alivyolinena. Halipaswi kuongezewa, wala kuondolewa, wala chochote kile, liamini namna hiyo.

90 Sasa, na wakati Ayubu akiwa nabii, hatimaye ono lilitokea, na basi alipoona jinsi ambavyo Mungu atamwekea mwanadamu njia ya kuishi tena, kwa sababu kungekuwako na Neno lingine lililonenwa ambalo bikira angelipokea.

91 Huyo alikuwa ni Hawa, kwanza, aliyelitilia shaka. Wakati Neno lilipomjia Mariamu, kamwe hakulitilia shaka, alisema, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu sawasawa na Neno lako." Mnaona, kamwe—kamwe hakusema, "Sasa, ngoja mpaka nitakapouhisi uhai, ndipo nitaenda kushuhudia. Ngoja mpaka niwe na hakika nalo."

92 Hivyo ndivyo sisi Wakristo, *tunavyojiita*, siku hizi tunavyofanya, "Ngojeni mpaka niwe na hakika. Ngojeni mpaka nitakapoanza kupata nafuu." Na, "Ngojeni mpaka nione jambo fulani likitukia, ndipo nitalifanya." La, bwana, hilo si—hilo silo swali, liamini kwanza.

93 Eliya alimwambia nini yule—yule mwanamke aliyemwendea, asiye na kitu ila konzi ya unga? Alisema, "Nitayarishie keki kwanza, kisha nenda uanze . . . " Mwujiza utatendeka baada ya wewe kulichukua Neno la Mungu kwanza. Wewe anza kuliamini Neno la Mungu, ndipo mwujiza utatendeka juu ya Neno, kwa sababu Neno ndilo Mbegu inayoleta mwujiza, huna budi kulichukua Neno kwanza. Roho Mtakatifu hulipa uhai, kama maji yanayoshuka kutoka Mbinguni.

94 Tunajua ya kwamba Roho Mtakatifu huwakilisha, uh, maji yanamwakilisha Roho Mtakatifu, kama, "Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba nyikani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa." Ati nini? Watu wanaoangamia. Naye alipomwinua yule nyoka wa shaba, iliyaokoa maisha ya

watu waliokuwa wakiangamia; wakati alipoupiga ule Mwamba, Kristo ndiye huo Mwamba uliopigwa, na kutoka Kwake yakatoka maji ya Uzima kwa ajili ya watu wanaoangamia. Huna budi kuliamini, kulifanyia kazi, sasa, kumbuka sasa.

95 Ndipo wakati Ayubu alipomwona huyu Mwenye *haki* akija, Yule ambaye angeweza kusimama katika pengo kati ya mwenye dhambi na Mungu, na kuiunganisha njia, Mbegu hiyo kamilifu, "Mbegu hizi," akasema, "zimeoza, ninaziona zikiingia ardhini. Wanawe wanakuja kumwomboleza, juu yake, yeye hajui. Analala pale, kamwe haamki, analala tu pale, anaoza, na ni hayo tu." Kamwe haamki tena, kwa sababu yeye ni mzao wenye dosari.

96 Lakini alisema, alipogundua ya kwamba kuna Mtu ajaye, Ambaye angerudisha ukamilifu kwenye Neno la Mungu tena, ambaye angefanya njia, angeiunganisha njia, ndipo huyo nabii akaingia katika Roho na kupaza sauti, "Najua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Alimwona Yule mkamilifu akija. Nini kilitukia? Ayubu, akiwa ni nabii, siri za Mungu zinajulikana kwa nabii, yeye alinena Neno, na wakati aliponena Neno ambalo Mungu alimwonyesha, likafanyika mwili, kwa kuwa lilikuwa ni Neno lililonenwa, na katika majira Yake, lilitukia vivyo hivyo hasa.

97 Kristo alizaliwa, Mkombozi, Yule, angeweza kusimama kati ya walio hai na waliokufa na kuiunganisha njia, na kuleta ufufuo, hasa. Kwa nini? Lilikuwa ni Neno la Mungu. Sasa, yeye alinena Neno, nalo hilo Neno lilikuwa ni Mbegu, Nalo likakomaa katika majira Yake. Kila Mbegu ya Mungu, ikiwekwa vizuri, itakomaa.

98 Sasa, vipi kama Mungu angetuma Ujumbe Wake, kwa Malaika, kwa Mariamu, na kusema, "Salamu, Mariamu, umebarikiwa miongoni mwa wanawake. Utapata Mtoto mchanga pasipo kumjua mwanamume," kama angesema, "Sasa, ngoja kidogo hapa, hebu nikupeleke kwenye maabara, nawe uniambie, hebu—hebu daktari anithibitishie jinsi nitakavyofanya jambo hili," mnaona, "ndipo nitakuamini"? Lisingetukia kamwe. Lakini aliishia wapi? Tumbo la uzazi la moyo wake, tumbo la uzazi ilimokuwa roho yake. Tumbo la uzazi la roho yako ni akili yako, nia yako ndiyo njia.

99 Una hisi tano zinazoutawala mwili. Una hisi tano zinazoitawala nafsi, dhamiri, na kadhalika. Sasa, mwili wako, kuna kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Lakini kuna njia moja tu ya kuingia ndani ya nafsi hiyo, inayoonyesha ya kwamba wewe ni Mzao. Wewe ni nafsi, mwili, na roho, na halafu njia moja, njia kuu, njia moja ya kuingia humo, uhuru

wako wa kujichagulia, yaani, unaweza kupokea au kukataa; unafanya lolote utakalo.

100 Kwa hiyo Hawa alikuwa kwenye msingi ule ule, angeweza kuchukua Neno la Mungu na kusema, "Mungu alisema tusifanye hivyo, na tuondoke hapa!" Hilo lingekuwa sawa, bali badala ya hilo alijaribu kulichanganya na uongo wa Shetani, na kumletea mauti. Lakini alipokuja kwa Mariamu, ilikuwa tofauti, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana." "Itakuwaje?" Hilo halijalishi jinsi itakavyokuwa. "Umelinena, ni Neno la Mungu, ninalipokea. Tazama mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu sawasawa na Neno Lako." Hilo hapo, hilo lilitosha, ndipo a—alikuwa sawa basi.

101 Mnaona, yeye alileta Chembe hiyo ya Uhai ambayo ilikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa katika umbo la mwanadamu. Na kupitia kwa kifo cha huyo Mwenye *haki*, ikalipiwa mauti kwa ajili ya ki-. . .deni ya kila mmoja wetu asiye na haki. Na kwa kukubali basi, Neno Lake, kunaleta Uzima na kumrudisha Kristo ndani yetu, kwa sababu Kristo ni Neno, Neno Lililonenwa. Nalo litakomaa kama unaweza kulipokea. Ninyi mlio wagonjwa, likubalini, liaminini, halina budi kukomaa, litatokea katika majira Yake, halina budi.

102 Sasa, sisi sote tunaamini ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Mtu yeyote ambaye, heh, ambaye ni mwenye akili, ninaamini, kama angeweza kuangalia kote na kuona, inaonyesha kitu hiki hakiwezi kuendelea muda mrefu zaidi. Sasa, ninataka yapata dakika kumi na tano sasa, kuwaonyesha ninalomaanisha. Mtu yeyote anajua ya kwamba jambo fulani halina budi kutukia, Maandiko yote yanaelekeza kwake.

103 Tunafundishwa ya kwamba ulimwengu uliumbwa katika miaka elfu sita, kukiwako na elfu moja kwa siku, siku moja kama mwaka kwa Mungu, na kadhalika, miaka elfu sita katika uumbaji. Vema. Zinaitwa siku sita, nayo Biblia inasema siku moja ni miaka elfu moja, ama, miaka elfu ni siku moja kwa Mungu.

104 Sasa, miaka elfu mbili ya kwanza ulimwengu, kosmosi, utaratibu wa ulimwengu, ulifikia mwisho wake, ndipo ilimbidi Mungu kutuma kitu fulani, zile hukumu kutoka Mbinguni, na kuihukumu dunia katika hukumu, na kuwaokoa wenye haki, Nuhu na familia yake.

105 Miaka elfu mbili ya pili, jambo lile lile lilitukia tena, kosmosi, utaratibu wa ulimwengu, hata Kanisa likachafuliwa. Siku za Nuhu, walimtania na kumdhihaki, naye akahubiri miaka mia moja na ishirini mlangoni mwa safina. Na katika miaka elfu ya pili Kanisa lingeninii. . .likaingia utumwani, likafanya uzinzi na ulimwengu, nalo likawa si kitu ila lundo la taratibu na kanuni za imani, ndipo Mungu akatuma hukumu

duniani kwa kumtuma Mwanawe, likafikia mwisho wa nguvu zake.

106 Sasa, huu ni mwaka wa 1962, nayo Biblia inasema nini? Biblia ilisema, katika siku za mwisho kwamba itabidi kazi ifupishwe, Maandiko hayawezi kusema uongo, kwa ajili ya Wateule, kwa ajili ya Wateule, la sivyo asingeokolewa mwanadamu yeyote. Ndipo tunaona tuko kwenye wakati wa mwisho.

107 Ya saba ni sabato, ambayo ni ule Utawala wa Miaka Elfu, huo ndio. . .huo utatukia katika wakati huo, ule Utawala wa Miaka Elfu. Sasa, lakini zile siku sita zimetimia. Mwanadamu anayo mkononi mwake, sasa hivi, silaha ambayo anaweza kujiangamiza mwenyewe, anaweza kuuangamiza ulimwengu, angeweza kuulipua ulimwengu vipande vipande katika sekunde moja. Anaweza kumrusha mtu kwenye mzingo, na kuizungusha kote humu nchini, na kusema, "Jisalimisheni, la sivyo nitaiachilia." Hivyo tu. Angefanya nini? Mbona, mtu yeyote mwenye busara, wangejisalimisha. Halafu nini?

108 Na sasa, maskini ninii. . .Ilikuwa kwamba mataifa makubwa yaliyatawala makubwa. . .mataifa madogo, sivyo tena, wana kitu kile kile. Mnaona? Kwa hiyo umekuwa wakati ambapo tunaona na kuamini ya kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho.

109 Sasa, tungeweza kuendelea na jambo hili kwa saa kadhaa, lakini hebu na tuangalie baadhi ya Maandiko hapa kwa dakika moja tu yanayoishughulikia ile Mbegu ambayo imepandwa kwa ajili ya wakati wa mwisho.

110 Kama Mbegu hiyo ya. . .Neno lililonenwa la Ayubu, Isaya alinena habari Zake, kila mtu wa Mungu, kila nabii wa Mungu ambaye alimjulisha siri Zake, hata Daudi, kufikia Isaya, Yeremia, hao wengine wote, walinena juu ya huo Uzao ujao, ndipo majira yalipowadia, ilikuwa hivyo hasa, Yeye hufanya hivyo daima. Haliwezi kushindwa, ni Neno la Mungu, ni la Milele, haliwezi kushindwa. Nasi sote tunajua ya kwamba Yesu alikuwa ni Neno.

111 Sasa, hebu tulichukue Neno Lake basi, Waebrania 1 ilisema, "Mungu zamani na kwa njia nyingi alisema na manabii, lakini katika siku hizi za mwisho kwa Mwanawe, Kristo Yesu." Sasa, Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii. Alikuwa ni Nabii, hakika, Musa alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii," lakini Huyu alikuwa ni zaidi ya nabii, Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili.

112 Sasa, huyu Mungu-Nabii alitupa ishara mbili ama tatu tunazotaka kuangalia hapa, ishara kuu tunazotaka kukumbuka. Katika Mathayo 24 wakati alipoulizwa "Mambo haya yatakuwa lini? Kuja kwa mwisho wa ulimwengu kutakuwaje? Haya yote yatatukia lini?" Alitoa mambo mengi sana mbalimbali ambayo

yangetukia, taifa litaondoka kupigana na taifa, ufalme kupigana na ufalme, na kadhalika, na kuendelea na kuendelea na kuendelea, bali akasema, "Jifunzeni mfano wa mtini, wakati . . . na miti mingine yote."

113 Ni wangapi hapa walio Wakristo sasa? Inueni mikono yenu. Kweli, asanteni, nakisia asilimia mia moja. Vema. Angalieni kwa makini sasa, tunapoileta ishara Mbegu hii ya wakati wa mwisho. Yesu alisema, "Jifunzeni mfano wa mtini. Sasa, mtakapoona mtini . . . " Sasa, mjifunze mfano wa nini? Mtini. Sasa, mtu yeyote anajua, anayesoma Biblia, ya kwamba mtini ulikuwa, daima umekuwa, jamii ya Kiyahudi.

114 Yoeli alisema, "Yaliyosazwa na tunutu yameliwa na madumadu," na kadhalika, hicho kilikuwa ni Kisiki, ambapo kanuni za imani na kadhalika zililiangamiza Kanisa, bali alisema, "Nitarudisha, asema Bwana."

115 Sasa, Wayahudi walikatiliwa mbali Paulo anatwambia, nao Mataifa wakapandikizwa tena, katika Ufalme, lakini, angalieni, Yesu alisema, "Jifunzeni mfano wa mtini." Sasa, mti huo, kama ule Ayubu aliouona, ukifa, je, utaishi tena? Hakika. Alisema, "Sasa, mtakapouona mtini, na miti mingine yote . . . " Miti, miti ya nini? Kuna Mti wa Uzima, kuna mti wa kanuni za imani, dhehebu, kuna kanuni ya imani ya taifa. "Mtakapouona mtini, na miti mingine yote ikichipuka," kutoa machipukizi, ikijiandaa kuchipusha majani, "mnasema majira ya kiangazi yamekaribia." Angalieni, akifanya mfano kutoka kwa mataifa.

116 Sasa, Mungu huwashughulikia Mataifa kama Bibi-arusi, mtu mmoja *hapa*, na mmoja *pale*, bali Yeye anawashughulikia Wayahudi kama taifa, sio kama mtu binafsi, kama taifa, amefanya hivyo daima, hilo limekuwa taifa teule la Mungu, Mungu aliwachagua kama taifa. Wamishenari wakiingia Yerusalemu, na kadhalika: wakati Israeli itakapookolewa, itakuwa "Taifa," Biblia inasema, "litazaliwa katika siku moja." Hiyo ni kweli. Kwa hiyo Israeli itamkubali Kristo mara moja, mara moja tu . . . kama taifa, sio tu kama watu binafsi.

117 Lakini, angalieni sasa yale Yeye aliyosema, hebu tuyachukue, tuyaangalie vizuri, "Mtakapoona mtini ukianza kuchipusha tena, na miti mingine yote ikichipusha majani yake . . . " Sasa, kila kitu kina uamsho, ama ndio kwanza kiwe na uamsho. Wayahudi wamerudi katika nchi ya uenyeji wao kama taifa, wakipeperusha bendera yao wenyewe, serikali yao wenyewe, pesa yao wenyewe. Wao ni taifa kwa mara ya kwanza kwa yapata, nakisia, yapata miaka elfu moja mia nane, loo, zaidi ya hiyo, yapata miaka elfu mbili mia mbili, kama miaka elfu mbili mia mbili, Israeli ni taifa tena. Bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni, ile nyota yenye ncha sita ya Daudi, inapepea tena, na kwa mara ya kwanza kwa miaka elfu mbili mia mbili, naye Yesu alisema, "Wakati litakapoanza kuchipusha machipukizi

yake, wakati umekaribia hata mlangoni." Israeli, akizungumza na Wayahudi.

118 Sasa angalieni, Yeye alisema, ". . . wakati miti mingine yote itakapoanza kuchipusha." Kanisa Katoliki la Kirumi limekuwa na mpanuko mkubwa sana lililopata kuwa nao, kanisa la Kiprotestanti limekuwa na uamsho mkubwa kuliko wote lililokuwa nao, Billy Graham, na Jack Shuler, Wapentekoste wamekuwa na uamsho mkubwa sana waliokuwa nao, Oral Roberts, Tommy Hicks na hao wengine, watu mashuhuri, uamsho.

119 Angalia, utawala umekuwa na uamsho, nguvu za kitaifa. Kuna uamsho unaoendelea sasa, "Ni nani atakayekuwa na uwezo mkubwa kuliko wote?" Ukomunisti, kila mtu, unawasikia wahubiri wakisimama mimbarani wakizungumza, "Loo, na tuogope ukomunisti!" Upuuzi. Nionyeshe Andiko ambapo ukomunisti utautawala ulimwengu; Urumi utatawala ulimwengu, sio ukomunisti. Angalieni lile ono la Mfalme Nebkadreza, Neno la Bwana, kile kichwa cha dhahabu, shaba na kushuka chini kuingia kwenye miguu ya Kirumi, ambayo ilikuwa ni chuma, wala haikubadilika kamwe. Lile jiwe lilikuja wakati ilikuwa ingali katika chuma na kuipiga. Kumbukeni mwishoni ilichanganywa na udongo, udhaifu, udongo na chuma pamoja.

120 Mkutano huu mkubwa ndio kwanza waufanye, hapa juu, kati ya Khrushchev na Eisenhower, je, mnajua *Khrushchev* linamaanisha nini katika lugha yake mwenyewe ya taifa? *Khrushchev* linamaanisha "matope, udongo." Mnajua maana ya *Eisenhower* katika Kiingereza? "Chuma." Na hata kulifanya dhahiri sana kwa watu, Khrushchev alivua kiatu chake na kupiga dawati; hawatakubaliana. Ni kitu gani kitakachotawala? Urumi utatawala. Mwungano wa makanisa, pamoja na Ukatoliki, utayaunganisha pamoja, na haya basi, mamlaka inayotawala. Biblia inasema ya kwamba, hiyo ndiyo ile Mbegu, isiyoweza kushindwa.

121 Sasa, angalieni siku hizi, huyu papa mpya si anayaalika makanisa yote ya Kiprotestanti yaingie ndani? Si wanaenda? Vipi kuhusu Wapentekoste wenu? Jambo lile lile, ule mwungano wa makanisa. Haya basi, hiyo mbegu haina budi kutimia. Hili halina budi kutukia. Halina budi kukomaa, ni wakati wake wa kukomaa. Hao watu, walifanya nini? Kuunda madhehebu na kuendelea kujenga majengo makubwa zaidi, na mashirika makubwa zaidi, madhehebu makubwa zaidi, basi yote yaliyotukia ni yapi? Jambo lile lile, vile vile hasa Biblia ilivyosema wangefanya.

122 Hivyo ndivyo Mungu-Nabii, Yesu Kristo, alivyosema ingetukia, Wayahudi wangerudishwa, na kungekuwa na uamsho mkubwa miongoni mwao kama taifa, wakikusanyika

pamoja kama taifa. Kutakuwako na uamsho miongoni mwa Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, na kadhalika, uamsho miongoni mwa Wapentekoste, na haya basi. Taifa litakuwa likipambana na taifa, ile mbegu imekomaa. Israeli imekuwa taifa baada ya miaka elfu mbili na mia mbili. Imekuwaje? Makanisa yote yalikusanyika pamoja yakifanya uamsho. Vema, bwana.

123 Sasa, Mbegu nyingine kuu ilipandwa. Yeye alisema, katika siku za mwisho, katika Timotheo wa Pili, mlango wa 3, kutakuja miongoni mwa kanisa kuanguka kutoka kwenye imani ya Biblia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni Mbegu? Hiyo ni ahadi? Waangalieni siku hizi, yaangalieni makanisa yetu. Yanafanya nini? Yanaungana pamoja, yanashirikiana pamoja, yakijifunga pamoja, yakishindwa, hayaiamini Biblia, hawaamini Neno ha—halisi la kweli la Mungu.

Unasema, "Biblia inasema *hivi*."

124 "Mambo hayo yamepita. Hakuna kitu kama hicho. Loo, ha—hakuna kitu kama hicho. Siku za miujiza zimepita, zamani sana. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, huo ulikuwa ni kwa ajili ya watu wachache, kumi na wawili huko nyuma, wale mitume." Mnaona? Mbegu hiyo ni nini? Inakomaa, ni ishara mbegu ya wakati wa mwisho.

125 Yesu alisema nini? "Mtakapoona mambo haya yakitendeka, inueni kichwa chenu, ukombozi wenu unakaribia," kwa Kanisa. Tuliona lingeanguka. Vema. Tunaona jambo hilo. Vema.

126 Sasa, tulisema, katika siku za mwisho, Yoeli alitwambia, ile sehemu nyingine ya Maandiko, sikilizeni kwa makini sasa, kwamba kungekuwa na mvua ya masika na mvua ya vuli katika msimu uo huo. Ni Wakristo wangapi wanaojua hilo? Semeni, "Amina." Hakika. Kitu gani?

127 Sasa, hivi majuzi, nilishangaa, nilipoangalia, mvua ya masika na ya vuli ingekuja katika msimu ule ule, sasa, neno *masika* katika, neno la Kiebrania, chukua kamusi yako ya Kiebrania uone, neno la Kiebrania la *masika* linamaanisha "moureh," *moureh* linamaanisha "kufundisha." "Kutakuja mvua ya mafundisho." Ni kitu gani? Kutia mbegu ardhini.

128 Kumekuwa na nini? Nini kimeendelea? Vema, tunaona ya kwamba kumekuwako na mvua ya mafundisho ikiendelea. Wabaptisti, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44," lilikuwa ndilo lengo lao, wafuasi wa kanisa. Miamsho mikuu ya Billy Graham, yule mwinjilisti mashuhuri, angalieni yale aliyofanya, mwangalieni Oral Roberts na Wapentekoste; kumekuwako na mvua ya mafundisho iliyoendelea.

129 Kumekuwako na mvua ya mafundisho ya kitaifa, ukomunisti uliopandwa miongoni mwa watu, kila taifa.

130 Kumekuwako na uamsho wa Kirumi. Mnajua kinachotukia? Wakirudisha sehemu ya magharibi, ama, sehemu ya mashariki ya Berlin, hilo linauweka ukomunisti ninii tu, ama, ninamaanisha himaya ya Kirumi, kabisa katika ile duara ya kale hasa ilimokuwemo katika wakati wa Yesu, bila shaka inafanya hivyo, kikamilifu.

131 Kuna uamsho unaoendelea. Ni kitu gani? Upanzi. Husikii sana kuhusu Billy Graham tena, sivyo? Vipi kuhusu Oral? Vipi kuhusu hao wengine? Mnajua ule moto mkuu wa uamsho hauwaki. Ni kitu gani? Ni ishara Mbegu ya wakati wa mwisho. Maneno yamepandwa. Ni kitu gani? Madhehebu yatavuna madhehebu, hilo linawafanya waungane pamoja.

132 Lakini Neno la Mungu limepandwa pia, basi wakati Roho wa Mungu atakapoanza kushuka, Neno la Mungu litaishi ndani ya watu. Na yule bibi-arusi wa uongo ambaye amefanya uzinzi huko nje, na kujiingiza katika kanuni za imani, na kuuza haki zake za mzaliwa wa kwanza atavuna nini? Mwungano wa kanisa, ambao hauna budi kufungwa na kuchomwa moto kama miiba na michongoma. Lakini ambapo Neno la Mungu limepandwa ndani ya mioyo ya watu, litavuna Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo, hakika kama ninavyosimama hapa. Ishara ya wakati wa mwisho.

133 Kuna shida gani, Kanisa la Mungu? Tuna shida gani? Mna shida gani ninyi Wabaptisti, ninyi Wapresbiteri, Assemblies of God, Jesus Only, ninyi wengine wote? Tuna shida gani? Hivi hamwezi kuona? Ile mbegu, usininii. . .kuwa mwangalifu unachukua mbegu ya namna gani katika tumbo la uzazi la moyo wako. Usichukue kanuni za imani, chukua Neno.

134 Wamekuwa wakizungumza sana kuhusu "mvua ya vuli." Si kuwatupilia mbali ninyi ndugu wa Mvua ya Vuli, bali hiyo si "mvua ya vuli," kama mvua ya vuli ingalikuwa hapa, nguvu za Mungu zingekipiga kitu hicho, nacho kingeenea kote ulimwenguni. Mvua ya vuli iko karibu kuja. Kuna shida gani? Kanisa linajitengenezea kitu fulani kama tu vile Hawa alivyojaribu kufanya, alijaribu kupata Nuru zaidi kutengeneza kitu fulani.

135 Tumefanya jambo lile lile, tukijaribu kufanya kitu ndani yetu wenyewe. Ondoa mkono wako Kwake, acha Mungu afanye hivyo, lichukue Neno Lake na kuliamini, lishikilie moyoni mwako, ndipo wakati mvua itakapoanza kunyesha Uzima utashika, nalo Neno litajidhihirisha Lenyewe.

136 Nadhani mnafikiri nina kichaa, lakini sivyo nilivyo; kama ndivyo nilivyo, niacheni, nina furaha hivi. Kwa hiyo, ninaamini Neno la Mungu. Kanisa lina shida gani? Tumbo lake la uzazi, akili ya—yake iliyo wazi, imepokea kila namna ya kanuni za imani na mafundisho ya sharti, wala si Neno la Mungu. Wakati Kristo alipokuja alikuta kitu kile kile Adamu alichopata, kitu kile kile Yehova alichopata. Na hizi hapa ishara hizi katika

wakati wa mwisho zikitokea, nalo kanisa halina jibu, hiyo ni kweli, wakati umewadia.

137 Mvua ya masika imenyesha, hiyo ndiyo sababu Billy hafanyi mengi. Kumbukeni, katika ninii kulikuwa. . . Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Kulikuwa na Malaika wawili walioshuka kwenda kwa Wasodoma. Kumbukeni, Lutu wakati mmoja alitembea na Ibrahimu. Kanisa wakati mmoja lilitembea katika ushirika pamoja na Kristo, pamoja na Neno, bali waliuza haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya madhehebu. Sasa, yeye anauza kitu hicho chote na kujiundia dhehebu katika mwungano mmoja mkubwa wa kanisa.

138 Hicho ndicho kilichompata Lutu hasa, alishuka akaenda kule, Malaika wawili, Oral Roberts, na Billy Graham, kama vile ingekuwa katika siku hii, walishuka wakaenda kule, na kuwawekea Injili. Ilikuwaje? Hata ilisababisha aibu.

139 Lakini Ibrahimu, Mtu mmoja alibaki nyuma pamoja naye. Kulikuwa na Mmoja ambaye yeye alimwita Mungu. Nayo ishara aliyofanya pale mbele yao, ilifanya nini? Ilithibitisha kile alichokuwa. Ibrahimu alikuwa ni Mteule, kwa sababu alikuwa. . . Ibrahimu alikuwa na ahadi. Na sasa angalieni, huu ni Uzao wa Ibrahimu, ahadi haikutolewa tu kwa Ibrahimu, bali Uzao wake. Si uzao wake Isaka, ulishindwa, ulithibitika ulishindwa, bali ule Uzao, imani aliyokuwa nayo, haidhuru hali ya mambo ilikuwaje, jinsi ilivyokuwa kinyume na maumbile, ni kiasi gani daktari alisema haikuwa hivyo, Ibrahimu, baada ya kupewa ahadi aliyopewa, wakati ilipokuwa haiwezekani.

140 Alimwoa dada yake mwenye umri wa kama miaka kumi na saba, dada yake wa kambo, hawakuwa na watoto, basi alipokuwa na umri wa miaka sitini na mitano naye mume alikuwa na sabini na mitano Mungu alimtokea na kusema, "Utapata mtoto kwake." Mbona, yeye alichukua. . . yeye alichukua Neno Lake, akajitayarisha kwa ajili yake. Miaka ishirini na mitano baadaye hakuna kitu kilichokuwa kimetukia, sasa yeye ana umri wa miaka mia moja, naye mke ana tisini, hilo halikumzuia hata kidogo, "Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini."

141 Hiyo ndiyo ile imani, huo ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, huo ndio aina ya Uzao unaolichukua Neno la Mungu, hicho ndicho kitu kitakachomleta Bibi-arusi, hicho ndicho kitu kitakachokutana na Kristo. Yeye ni Neno.

142 Na kama Kanisa limepandwa na kitu kingine mbali na Neno, haliwezi kwenda kukutana na Yeye. Hana mwili wa ajabuajabu wenye ukungu, Yeye ana Mwili mkamilifu, Naye ni Neno kamilifu. Nalo Kanisa litapandwa na kuamini Neno kamilifu. Ndipo Neno kamilifu na Neno kamilifu vitaungana pamoja kama nyama moja na Mwili mmoja, kama vile mume

na mke walivyo. Amina. Sijiitikii amina mwenyewe, bali *amina* linamaanisha “Na iwe hivyo.” Ninaliamini, kwa vyovyote vile. Naam, bwana.

143 Mvua ya masika imenyesha. Mvua inakaribia kunyesha. Itazaa nini? Angalieni tu.

144 Ishara moja zaidi: yule mwanamwali mpumbavu. Yesu alisema, kabla tu ya kuja kwa Bwana-arusi kungekuwako na mwanamwali mwenye busara akiwa na Mafuta katika taa yake, na yule mpumbavu. Naye mwanamwali mpumbavu angeamka siku moja na kuona kwamba hakuwa na Mafuta yoyote katika taa yake, wakati ilipofikia mahali, “Tazama Bwana-arusi yuaja.” Hivyo ndivyo ile sauti ilivyo sasa, “Kristo yuaja.” Ndipo akaamka na kugundua kwamba hakuwa na Mafuta yoyote.

145 *Mafuta* maana yake ni “Roho.” Roho ndiye anayelipa Ne—Neno Uhai. Roho ni Maji yanayolipa Neno Uhai. Mtupe nje, useme, “Vema, vipi kuhusu makanisa haya?” Kama yakipanda mbegu za kimadhehebu Huyo atalihuisha hilo, Roho wa Mungu atalihuisha hilo.

146 Biblia ilisema, “Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki.” Waebrania mlango wa 4. . ., uh, wa 3. . .mlango wa 6 unasema ya kwamba mvua huja mara kwa mara ili kustawisha matunda yaliyo ya nchi, bali miiba na michongoma ambayo ilishangilia vivyo hivyo na kuishi kwa mvua kadiri iwezavyo. “Bali kwa matunda yao mtawatambua.” Hiyo ni kweli kabisa. Haya basi. Sasa, walipoona hayo. . .Mnaona, matunda yanapaswa kukusanywa, mvua iko karibu kunyesha. Madhehebu yataangua madhehebu, hivyo tu. Lakini Neno litamwangua Kristo, Bibi-arusi, bila shaka. Panda Neno la Mbegu. Sasa, wakati yule mwanamwali mwenye busara. . .

147 Mmeona *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo? Ninazungumza kwa niaba yao kimataifa, siwezi kuwabembeleza, Hili ni Neno. Angalieni, vipi kuhusu. . .? Angalieni hapa kwa Wapresbiteri, Waepiskopolia, mamia yao, kila mahali, wakijaribu kumtafuta Roho Mtakatifu. Wanatimiza jambo kubwa mno.

148 Mhudumu rafiki yangu wa thamani kutoka Afrika, mtu mzuri, mtauwa, nimemwuliza, “Hivi hujui ni kitu gani, Ndugu? Huduma yako ni ipi?”

Akasema, “Ninapaswa kuingiza Babeli.”

149 Nikawazia, “Hivi huwezi kuona, wakati ule ule ambapo yule mwanamwali mpumbavu anapotaka Mafuta kuzifanya mbegu zake zikue pia, huo ndio wakati Kristo anapokuja naye anaachwa nje?”

150 Yule mhubiri mashuhuri Billy Graham ndio kwanza aseme ya kwamba tunahitaji Pentekoste, tunahitaji watu warudi. Waepiskopolia waliandika makala nzuri sana, folda ndefu

*hivi*, kasema, “Tunahitaji wenye kunena kwa lugha. Tunahitaji waponyaji wa Kiungu Kanisani wakiwa na ibada za uponyaji, watu huko nje wakiwaombea wagonjwa.” Wanajaribu kufanya nini? Kutia Mafuta katika taa yao, kweli kabisa. Hiyo ni ishara Mbegu ya wakati wa mwisho. Amina. Wakati alipokuwa akijaribu kufanya hivyo, Bwana-arusi akaja naye Bibi-arusi akaingia, huyo akafungiwa nje. Loo, ni siku nzuri jinsi gani tunayoishi!

151 Ninataka tu kusema jambo moja zaidi: dhiki kati ya mataifa. Loo, jamani! Mambo yasiyo ya kutisha mbinguni, mnaamini ndivyo ilivyo? Angalieni, tunachukua tu baadhi yake. Je, tuna dakika zingine chache, kumalizia saa tatu na nusu? Sitaki kushikilia hili jumba la mikutano. Sisi . . . Kuna neema kwa watu hawa, kuturuhusu tulichukue.

152 Sikilizeni, ni wangapi, na kila mmoja wenu, mmeona taifa limetikiswa hivi majuzi tu kuhusu ishara. Mliona yale, mtu huyu kwenye ule mzingo hivi majuzi? Aliona vitu huko juu asingeninii, sayansi hata haijui ni nini, wakati alipoizunguka dunia, hata hivyo wamechunguza na kuchunguza na kuchunguza, bali hawakuviona, alidhani mzingo wake utavunjika vipandevipande, haikutukia, mzingo wake ulikuwa sawa, nuru mbalimbali.

153 Angalieni kile ambacho kimekuwa tu kwenye . . . mmekiona kwenye redio, mlikiona kwenye televisheni, kimekuwa kwenye gazeti, visahani virukavyo kila mahali. Nayo Pentagoni ilivitangaza hivi majuzi, yapata majuma sita yaliyopita, hayakuwa ya kubuniwa, hata walilionyesha kwenye televisheni jinsi walivyoshika visahani hivi, vyenye akili, nuru zilizoshuka, zikining’inia juu ya Pentagoni namna hiyo, kote katika Washington, DC, nao wakavinasa kwenye rada, navyo vilikuwa na marubani kule juu, nao wangeingia moja kwa moja karibu navyo, wavizunguke, waondoke kwa mwendo wa radi, akili. Ni kitu gani?

154 Yesu alisema kutakuwako na ishara za kutisha, mambo ya kutisha mbinguni, mioyo ya watu ikivunjika, hofu, fadhaa za nyakati, dhiki kati ya mataifa. Hivi hamwoni kwamba wakati wa Mbegu umewadia sasa, wakati wa mavuno, mambo ambayo Biblia ilisema yangetimia? Hiyo Mbegu ambayo imepandwa, hivi hamwoni Hiyo imepata uhai na inaishi? Hiyo ndiyo shida.

155 Sasa, jambo moja tu zaidi, sikilizeni, hapo awali, sasa sikilizeni kwa makini, msikose kuliona hili sasa, kabla ya kule Kuja mara ya kwanza kwa Yesu, wale wanajimu wa India, Mamajusi, nimefanya umishenari huko India, na kuzungumza na Mamajusi kuhusu hili, nao walikuwa wakiangalia, walikuwa mamajusi, walikuwa wakiangalia sayari za mbinguni. Nao wanasema Mungu daima hujitangaza Mwenyewe katika sayari

za mbinguni kabla hajafanya hivyo duniani, kabla hajafanya lolote.

156 Nao wakasema, “Mbona, wakati hawa, wale mamajusi watatu walipoenda kumwabudu Mfalme huyu ambaye angeitawala dunia, Mfalme mchanga, kwamba waliifuata nyota, Maandiko yako yanasema.” Akasema, “Lakini kwa kweli, kulikuwako na nyota tatu zilizoungana pamoja na kuifanyiza nyota hii moja.” Nao wanasema, “Huyo. . . ” Mkristo mnajimu niliyekuwa nikizungumza naye, ama, majusi, alisema, “Hiyo inamaanisha kwamba kulikuwako na jamii tatu za watu ambazo Mtu huyu alizifia. Jamii tatu pekee zilizopo, ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, na wakati Injili Yake imehubiriwa kwa watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, watakapokuja pamoja katika Injili Yake, basi kule Kurudi kutatimia.”

157 Hilo ni sawa kama anataka kuamini hilo. Tatu ni namba ya ukamilifu. Lakini ninaamini hao watatu walikuwa nini? Tunaamini nini? Ilikuwa ni tatu ya ukamilifu ikionyesha ya kwamba utatu wa Mungu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ulidhihirishwa katika Mwanadamu, Yesu Kristo, yule Mtu mmoja mkamilifu. Watu wengine wote walikuwa wameshindwa, vingine vyote vilikuwa vimekufa, bali huyu hapa anakuja Mtu asiyeweza kufa, ukamilifu, ambaye hata mauti isingeweza kumwua, akafufuka tena.

158 Tatu ni namba ya ukamilifu, sote tunajua hilo, tatu ni namba ya Mungu katika numerolojia Yake. Mungu anajulikana kwa namba Zake, tatu ni ukamilifu, na saba ni ibada, ishirini na nne ni ibada, arobaini ni majaribu, hamsini ni Pentekoste, yubile, mnaona, na kadhalika. Nambari Zake zote, tarakimu Zake za Mungu zimekamilika, ziko katika ukamilifu. Sasa, tatu ni namba ya ukamilifu. Kabla tu wakati ninii, sikilizeni sasa kwa makini, wakati mtoto mchanga Kristo alipozaliwa, nyota tatu zilienda pamoja na kuifanya ile nyota moja ya asubuhi, ambayo iliakisi kule Kuja kwa mtoto Kristo, Mkamilifu.

159 Sasa, imekuwaje? Tunaona mngurumo kwenye gazeti, kote kupitia televisheni kote katika mataifa, ambapo nyota tano zilipanga mstari pamoja na ulimwengu. Tano ni nini? Nambari ya neema. Kila wakati nyota hizo zinapokuja, basi jambo fulani linatukia duniani. Ni kitu gani kilichotukia? Nyota tano ziliingia mstarini. Ilikuwa ni nini? Ku—kutambulishwa kwa kitu gani?

160 Tangu wakati huo, angalieni tu yale yaliyotukia, Ujerumani nusura iangamizwe kabisa, baadhi ya Mamajusi walisema ya kwamba ulimwengu ungepasuka kama tikitimaji, kila mambo ya dhiki ambayo wameyatabiri kwa ajili ya siku za mwisho. Angalieni yuliyotukia, Uingereza, hivi majuzi, ilikuwa na dho—dhoruba iliyozipeperusha nyumba sabini elfu, siku moja. Maafa kila mahali, California, Los Angeles karibu kuzamishwa baharini. Ni kitu gani? Mwanzo wa huzuni. Matetemeko ya ardhi

yameongezeka kila mahali. Ni kwa nini? Nyota tano zilipanga mstari, neema, neema ya Mungu.

161 Imekuwaje? Kanisa changa, haleluya, Bibi-arusi, uchanga, ambaye nguvu za Mungu zimeanza kumshukia, anaumbika, Bibi-arusi kwa ajili ya Bwana-arusi huyu. Hizo nyota tatu zilimaanisha ukamilifu Wake wa Baba wa Mbinguni, wa utatu kuwa Mmoja duniani miongoni mwetu, ofisi za Mungu zikifanyika ofisi moja. Ni kitu gani kilichotukia sasa? Ni Kanisa la Mungu aliye hai likija pamoja chini ya Neno la Mungu, na mbingu ya elimu ya nyota inatangaza kukaribia Kwake. Amina. Huenda usiamini hilo, bali ni Neno vile vile tu. Naam, bwana.

162 Ni kitu gani kinachotukia? Ninafunga, huenda nikasema hivi: Marafiki, Kanisa linakuja. Mungu atakuwa na Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi, Nalo limekusudiwa tangu zamani, Mungu alisema hivyo, Yeye atakuwa Nalo, hilo hulifanya sahihi. Mshiriki ni nani? Sijui. Ninatumaini kuwa mimi mwenyewe, ninatumaini wewe ni mshiriki. Lakini Yeye atakuwa na Mwili usio na waa wala kunyanzi.

163 Nami ninaamini ya kwamba ishara hizi za siku za mwisho na kadhalika zinazotendeka, kila moja yazo inajitokeza kuonyesha ya kwamba Kristo yuko tayari kumjia Bibi-arusi huyu. Kama vile Mungu katika Neno Lake alivyodhihirishwa katika Mtu, Mtu mkamilifu, vivyo hivyo Mungu na Neno Lake wanakuja tena, na kujidhihirisha Mwenyewe katika Bibi-arusi. Hatafanya kama Hawa alivyofanya, kulichanganya na kitu kingine, bali Neno la Mungu lisiloghoshiwa litazaliwa katika Kanisa hilo, Nalo litasimama kama Yesu Kristo alivyofanya, kwa upako wa Roho Wake katika Neno Lake. Amina. Ninaamini ni tangazo sasa.

164 Nabii alisema, "Itakuja siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru." Ninyi nyote wasomaji wa Biblia mnajua hilo. Ni nini kilifanyika? Ustaarabu husafiri kutoka mashariki hadi magharibi. Uchina ndio ustaarabu wa kale kuliko wote tulio nao. Ustaarabu ulianzia mashariki, umeambatana na jua, ukisafiri magharibi. Uko wapi sasa? Pwani ya Magharibi; ukienda mbali zaidi umerudi mashariki tena. Mnaona ninalomaanisha?

165 Jua lile lile linalochomoza mashariki ndilo jua lile lile linalotua magharibi, j-u-a lile lile. Na M-w-a-n-a yule yule, Mwana wa Mungu aliyekuja duniani kuchukua bibi-arusi kwa watu wa mashariki, naye bibi-arusi huyo akajichafua kama Hawa alivyofanya, kama bibi-arusi wa Yehova alivyofanya, Mwana yuyo huyo anayeangaza kule, aliyeangaza kule kwa nguvu Zake zile zile juu ya Pentekoste, kuivisha Mbegu ambayo Yeye alikuwa ameipanda, Mwana yuyo huyo anaangaza sasa katika ulimwengu wa magharibi. Kufanya nini? Kuivisha Mbegu ambayo imepandwa ipate kumzaa Bibi-arusi. Nuru ya jioni ya

Injili itamzaa Bibi-arusi, amina, kwa ajili ya Bwana Yesu. Hizo hapo baadhi ya ishara Mbegu za jioni, mamia yake.

166 Tuna dakika tano kabla ya kufunga. Je, wewe ni mmoja wa wa-. . .? Unaamini wewe ni mmoja wa hizo Mbegu? Unaamini ya kwamba moyo wako umepandwa Injili isiyoghoshiwa, hakuna kitu ulimwenguni kinachoweza kuliondoa Neno la Mungu moyoni mwako? Unaamini hilo? Kama sivyo, rafiki yangu, huenda nisikuone tena juu ya uso wa dunia hii, lakini kumbuka: Neno la Bwana na siri ya Bwana hujulishwa manabii Wake, manabii Wake walinena habari Zake, Hili hapa papa hapa sasa, tunaliona likitimia, ninarudia yale waliyosema katika kuwaonya ninyi.

167 Kama huna hizo Mbegu, na kama uko hapa usiku wa leo, nawe si Mkristo, wewe, labda wewe ni mfuasi wa kanisa, usibahatishe, ndugu, usisikilize mambo hayo, hayo ni mambo chotara, Neno la Mungu halina budi kuishi ndani yako kwa ukuu sana, kama lilivyofanya katika Yesu Kristo, kwa kuwa Yeye ndiye Kichwa, Mwili Wake hauwezi kuwa kitu *kimoja*, na Kichwa Chake *kingine*, hauna budi kuwa ni Neno lile lile. Kama kanisa lako linakuandalia tu kanuni za imani na mafundisho ya sharti ambayo si ya Kimaandiko, usiyaamini. Huwezi kuunganishwa katika kanisa, unazaliwa katika Mwili kwa Neno la Mungu aliye hai. Na kama huna hilo, usibahatishe.

168 Kama ulishuka hapa ku—kununua bakuli la supu, nayo ilikuwa na buibui ndani yake, ungeushtaki huo mkahawa. Mbona, usingeinywa kamwe, kwa sababu unahofu itauangamiza mwili huu. Ndugu, usiogope kile kinachoweza kuuangamiza huu mwili, bali Yeye anayeweza kuangamiza ninii, nafsi na mwili kuzimuni. Kama wewe ni mwangalifu sana kuhusu chakula chako, usingekula chochote kichafu kuufanya mwili huu uugue au kudhoofika, na halafu umeze aina yoyote ya kanuni ya imani kwa ajili ya nafsi yako ambayo ni ya Milele, wakati mwili huu hauna budi kuangamia? Usimwache ibilisi ashindilie upuuzi huo kooni mwako.

169 Wewe zaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, ndipo roho yako itashuhudia kwa kila Neno aliloandika Mungu *Hapa*, ndipo kila ahadi aliyotoa itajidhihirisha ndani yako. Roho wa Mungu atakuja na kuishi ndani yako. Wewe ni Mwili wa Kristo, uwakilishi Wake hapa duniani. Kama huna huo, kama huwezi kuamini kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu. . .

170 Kama uko hapa na ni mgonjwa, nawe unaamini ya kwamba Mungu atakupa uponyaji wa Kiungu, liweke tu hilo Neno, "Mimi ni Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote." "Bwana, ninaamini." Angalia kitakachotukia. Sema, "Bwana, ninaamini," fungua kila mkondo, "nami huyu hapa." Angalia kinachotukia, kama nilivyofanya, maskini msichana

huyo aliyekuwa akifa hivi majuzi, maelfu ya wengine kote ulimwenguni.

171 Nilisimama na kuwaona karibu na...Niliona...Huko Afrika Kusini niliomba ombi moja juu ya kundi la watu, nao wakakadiria, wakachukua malori saba makubwa yaliyojaa... Jamani, hamna lori huku Georgia kama moja ya hayo, karibu magurudumu sita ama nane kote hapa! Na kesho yake asubuhi, huku meya wa mji ameketi pale, alikuja dirishani na kusema, "Ndugu Branham, shuka, angalia *hapa*." Wakishuka kuja barabarani, hao hapo wakishuka barabarani wakiwa na malori saba yaliyojaa magongo, na viti vya magurudumu, na—na kila kitu watu ambao...

172 Sikumgusa hata mmoja wao, nilililete tu Neno, nikawaambia waliamini, nao wakaliamini. Nao watu waliokuwa katika vitu hivi siku iliyotangulia, hawa hapa wakitembea barabarani huku wameweka mikono yao juu ya moyo wao, katika lugha yao ya kienyeji wakiimba, "Mambo yote yanawezekana, Amini Tu."

173 "Yeye alilituma Neno Lake," hilo tu ndilo unalofanya ni kulituma Neno nalo Kanisa linalipokea. Yeye aliyezaliwa na Mungu humpokea Mungu, humwamini Mungu. Mnamwamini? Na tuinamishe vichwa vyetu. Nitaziombea leso hizi.

174 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa na kila jicho limefumbwa, ningetaka kuwaulizeni swali zito. Kama huko vizuri na Mungu, kama kuna kitu fulani ndani yako, kinachokuzuia kuamini Biblia hii kuwa ni Neno la Mungu lililovuviwa, usingeweza kuamini ya kwamba ungeweza kuishi kulingana na kanuni Zake, je, waweza angalau kuinua mikono yako, na kusema, "Mungu, nirehemu. Nataka uniombee, Ndugu Branham, kwamba nitakuwa Mkristo wa namna hiyo." Mko hapa? Inueni mikono yenu. Mimi...Asante, Msichana, asante, Mungu akubariki. Vema. Kuna mtu mmoja humu jengoni anayewazia hilo, wawili kati yao wanaowazia hivyo.

175 Mimi—mimi si mmoja wa watu hawa wa kushawishi kama Neno haliwezi kulisogeza. Unaweza tu kufanya hivyo wakati umechaguliwa tangu zamani kuliamini. Mnakumbuka, ingawa Yesu alifanya miujiza mingi sana, Mafarisayo wasingeweza kuamini jambo Hilo, wasingeweza kuliingiza kichwani mwao, kwa sababu hawakupaswa kuwa hivyo. Na kama moyo wako ni mgumu sana hata unajua papo hapo kwamba Neno hilo la Mungu halifanyi kazi kupitia kwako, halafu hutamwinulia Mungu mikono yako kuomba rehema, utafanya nini kwenye Siku ya Hukumu? Vema.

176 Je, kunaweza kukawa na mtu mgonjwa ambaye angetaka kukumbukwa? Inua mkono wako. Watatu ama wanne, watano, sita, saba, wanane, yapata watu kumi.

177 Vema, hebu na tuinamishe vichwa vyetu. Usitie shaka. Wewe, maskini dada yangu huko nyuma aliyeinua mkono wake, "Unikumbuke," Mungu akubariki, Dada, aubariki moyo wako mchanga. Neno la Mungu na lipate mizizi katika maskini moyo wako usiku wa leo, upate kuwa mmishenari kwa Kristo.

178 Mtu huyu aliyeinua mikono yake baadaye kidogo hapa, Ndugu, nywele zako zina mvi, lakini kumbuka Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano kabla Mungu hajanena naye. Mungu na apande mizizi Yake ya Neno moyoni mwako usiku wa leo, wakati mvua kuu inaponyesha, jalia isilete tu kanuni ya imani, jalia imzae Kristo aliyedhihirishwa ndani yako.

179 Kila mmoja wenu aliyeinua mkono wake kwa ajili ya uponyaji, Biblia ilisema, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, naye Mungu atawainua." Kama Mbegu imekaa moyoni mwako, nitaomba ya kwamba Roho Mtakatifu ataitia hiyo Mbegu maji sasa hivi; jambo fulani litatukia.

180 Mungu hana upendeleo, kama atamwokoa mmoja, atamwokoa huyo mwingine atakayeliamini. Kama akimponya mmoja, atamponya huyo mwingine, bali huna budi kuamini. Kama unaamini, nitakuombea sasa.

181 Baba yetu wa Mbinguni, nimeweka mkono wangu juu ya leso zilizowekwa hapa. Mtu fulani ana, labda, ana mpendwa mahali fulani ambaye ni mgonjwa na anateseka, wana shida fulani, labda mama mahali fulani na mtoto mchanga, mgonjwa, labda mzee, baba kipofu, ameketi nyuma kwenye kibanda kidogo hapa nje mahali fulani huko Georgia, labda mmoja hospitalini mahali fulani; Nawe unajua yote kuhusu mambo haya. Bwana, tunajua jambo hili moja, ya kwamba Wewe ndiwe Kristo ambaye tayari umenunua uponyaji wao. Ninalituma Neno Lako kwa njia ya maombi, Bwana. Ulilituma Neno Lako.

182 Yule mwanamke alikuja Kwako, akasema, "Bwana, unirehemu, Ewe Mwana wa Daudi." Nawe hukuwa Mwana wa Daudi kwake, yeye alikuwa Mmataifa. Yeye . . .

Ulisema, "Si vema Kwangu, kukitwaa chakula cha watoto, na kuwapa mbwa wenu."

Akasema, "Hiyo ni kweli, Bwana, lakini mbwa watachukua makombo kutoka chini ya meza ya bwana wao."

183 Ukasema, "Kwa msemo huu binti yako ataishi." Nasi tunaona ya kwamba ulipofika nyumbani, ama, alipofika nyumbani, Neno Lako lilikuwa tayari limefika kule, likamponya msichana huyo.

184 Baba fulani wakati mmoja, kwa ajili ya mtoto wake, aliuliza ilikuwa ni saa ngapi. Kasema, "Yapata saa kumi na moja ile homa ilimwacha," Wewe ulituma Neno Lako. Bwana, ninatuma Neno Lako kwa maombi ya imani, ninalituma kwa yule msichana mdogo pale aliyeinua mkono wake, Ninalituma

kwa mtu yule aliyeinua mkono wake, jalia lishikilie, usiku wa leo, kwa ajili ya wokovu. Tujalie, Bwana.

185 Sasa, Wewe ulisema, "Yeye aaminiye . . . ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele." Sasa, Bwana, hilo ni Neno Lako, Wewe ulisema hivyo.

186 Kulingana na sayansi, walivunja kila kanuni, sayansi inasema huwezi kuinua mkono wako, nguvu za uvutano zinaushikilia chini. Lakini kuna roho ndani ya mwanadamu, anaweza kufanya uamuzi na kuinua mkono wake, kwa sababu kuna roho fulani inayomtawala, inayozivunja kanuni za sayansi. Sasa, Mungu alinena, nao wakainua mkono wao kuelekea kwa Mwumba wao. Baba wa Mbinguni, jalia Neno Lako lianguke mioyoni mwao sasa hivi, liingie kwenye tumbo la uzazi la moyo wao, na kuleta, kupitia kwao, Bibi-arusi wa Kristo. Tujalie, Baba.

187 Kwa hawa walioinua mikono yao ambao ni wagonjwa kwenye jengo hili hapa, waliinua mikono yao kwa sababu wao ni wahitaji, wanakuamini Wewe kuwa ni Mponyaji. Sasa, ninaomba maombi haya ya imani, ninayatuma, Bwana, Katika Jina la Yesu Kristo, imani hiyo na ianguke katika kila moyo sasa hivi. Jalia Neno la Mungu liwe hapo kwa mkazo sana hata litaleta uponyaji kwa kila mmoja wao. Tujalie, Baba.

188 Sasa, tena, nasema kwa ajili ya leso hizi zilizowekwa hapa, katika Biblia ilisemwa walichukua kutoka katika mwili wa Paulo leso na nguo, ndipo pepo wachafu wakawatoka watu, magonjwa yakatoweka. Sasa, sisi si Mtakatifu Paulo, bali si yeye aliyefanya hivyo, kwa sababu ndani yake mlikuwamo Neno, Wewe ungali ni Neno lile lile.

189 Sasa, Baba, wakati mmoja Israeli walipokatiliwa mbali kutoka kwenye nchi ya ahadi, ilikuwa ni bibi-arusi wako, ulikuwa umemweka njiani kuelekea nchi ya ahadi, ulikuwa ukimtengenezea njia, adui akawazuia, uliangalia chini kupitia ile Nguzo ya Moto kwa macho ya hasira, bahari ikaogopa, ikarudi nyuma, Israeli wakasonga mbele.

190 Sasa, Mungu, si kuangalia kupitia Nguzo ya Moto, bali angalia kupitia Damu ya Mwanao Mwenyewe, Ambaye alikufa kwa kusudi hili, nami ninatuma Neno Lako, jalia ibilisi aogope, jalia aondoke, na jalia watu hawa waje kwenye ahadi hiyo ya Mungu, kama vile Israeli walivyofanya, bila kushindwa hata kidogo, jalia waje kwenye ahadi ile kuu, "Zaidi ya yote nataka mfanikiwe katika afya." Tujalie, Bwana. Jalia Hili lifanye kazi mahali tunapolituma, tukisema ya kwamba Neno Lako halitarudi Kwako bure, Litatimiza kile lilichokusudiwa. Nami ninaomba maombi haya ya imani kwa ajili ya watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo.

191 Sasa wakati tumeinamisha vichwa vyetu, ni wangapi wenu sasa watakubali yale yanayosemwa, na kuamini ya

kwamba Neno la Mungu limewajilia, nanyi mnalikubali, kila mtu uliyeinua mkono wako, haidhuru ulikuwa ni wa nini, utainua mkono wako, useme, “Ninaamini, ninalikubali sasa hivi, ninaamini nina kile nilichoomba”? Mungu awabariki, hilo ni zuri sana, hilo ni jema. Mungu awabariki. Ninatumaini ya kwamba Neno la Mungu litapata mizizi ndani yenu.

192 Sasa, inakubidi, wakati umeinamisha kichwa chako, mna mchungaji hapa, ndugu mpendwa, aje hapa na ku—kunukuu kama alivyofanya dakika chache zilizopita. Mwinjilisti hapaswi kushughulikia yote mkutanoni, lazima mumjue mchungaji wenu, mtu huyu mtauwa. Nina furaha sana kuwafikia watu hawa walioinua mikono yao kwa ajili ya mambo haya, na kuwapa mchungaji huyu mzuri sana. Hebu na awaongoze sasa kwenye kilindi cha ujuzi zaidi wa Mungu kwa ajili ya uponyaji na wokovu wenu. Mungu akubariki, Ndugu, Mchungaji. [Mchungaji anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Chochote tu utakacho baada ya kuomba.

62-0319 Ishara Mbegu Ya Wakati Wa Mwisho
Tifton Junior High School
Tifton, Georgia Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org